

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

BUNGE LA KUMI NA MOJA

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Sitini – Tarehe 5 Julai, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae Waheshimiwa. Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunayo Taarifa ya Spika, katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha ya mwaka 2017 yaani *The Appropriation Bill 2017*; na

(ii) Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 i*The Finance Bill 2017*).

Kwa taarifa hii napenda kurialifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa sheria za nchi. Kwa hivyo sasa tuna Sheria inayoitwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Na. 3 ya mwaka

2017 (*The Appropriation Act No. 3 of 2017* na Sheria ya Fedha Na. 4 ya mwaka 2017 (*The Finance Act No. 4 of 2017*).

Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana kwa kazi nzuri na kwa kuwa Sheria hizi sasa zimeanza kazi naamini utekelezaji wa yale ambayo Bunge limeyapitisha umeshaanza tangu tarehe 01 Julai, 2017 aliposaini Mheshimiwa Rais. Baada ya hayo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2017*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI (K.n.y. MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No. 1 of 2017*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y MHE. TUNDU
A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2017*).

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Maswali tutaanza na Wizara ya Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Boniphace Mwitwa Getere, Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake.

Na. 497

Miradi ya Maji Mugeta/Nyang'aranga na Nyamuswa

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Miradi ya maji ya Mugeta/Nyang'aranga na Nyamuswa ambayo inadhaminiwa na Benki ya Dunia imeshindwa kumalizika tangu mwaka 2013 hadi leo.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi hii kwa ufanisi na kukabidhi kwa watumiaji?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya ahadi ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Makala akiwa Bungeni ya ukaguzi wa miradi hii hususan mradi wa Mugeta ambao una bajeti mbili kwa mradi mmoja?

NAIBU WA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji inatekeleza miradi ya maji chini ya Programu ya Maendeleo ya Maji (*WSDP*) ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inatekeleza Miradi kwenye Vijiji 10 vikiwemo Vijiji vya Mugeta/Nyang'aranga na Nyamuswa. Jumla ya miradi mitano ya Karukekere, Mumagunga, Kung'ombe, Mugeta na Ligamba imekamilika. Miradi ya Nyamuswa, Nyamatoke, Kibara, Bulamba na Kinyambwiga ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Mugeta umekamilika na hivi sasa wananchi wanapata huduma ya maji isipokuwa Kitongoji kimoja cha Manyangale ambacho kitapata maji kutoka chanzo kingine baada ya kufanyiwa usanifu mwezi Agosti, 2016. Ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Nyang'aranga umekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu ulikuwa unatumia bajeti mbili, tayari Mkoa wa Mara umechukua hatua kwa kuunda timu ya wataalam kukagua na kuchunguza jambo hilo. Pindi ripoti hiyo itakapotufikia, basi hatua stahiki zitachukuliwa.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ambayo nimepewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kusema kweli sijui Bunda kuna nini hata nashindwa kuelewa. Kwa sababu unapotaja Kijiji cha Karukekere, Mumagunga, Kung'ombe, Ligamba na kama unavyotaja majibu kwenye *paper* ambayo nimepewa

kwa maana ya kujibiwa kama Mbunge, yakaonyesha sehemu kubwa ya miradi inayotajwa sio ya Jimbo lako, hivi Mbunge unajisikiaje!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba ni vizuri wakati fulani haya majibu, na nazani hili ni tatizo la Bunda tuna miradi mikubwa iko Bunda na Mabilioni ya hela, viongozi hawafiki pale kuona hela zinaliwa pale hawafiki, sasa naomba kuuliza niache kwa sababu leo ni siku nzuri tunaenda nyumbani tusilete shida huko mbele niseme sasa nimuulize Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuache haya ambayo ameyasema kwa sababu mimi sioni kama yako kwenye maeneo yangu, kuna kilometa nne za mradi wa maji mkubwa kutoka Ziwa Victoria huko Halmashauri jirani ya Butiama, sasa kama ni kilometa nne kuja kwenye maeneo ambayo yana uhaba wa maji ni lini Serikali itachukua mpango wa kuleta yale maji kutoka bomba la Ziwa Victoria kuja Nyamuswa, Bigegu, Tiring'ati na Malambeka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa kuna mradi mkubwa ulikuja wafadhili kutoka *SNV* wa shilingi milioni 987 kuja Kijiji cha Nyamuswa na mradi ule unaonekana umefanyiwa ubadhirifu mkubwa sana ni lini Serikali itaenda kushughulikia wabadhirifu wa hela hizo?

NAIBU SPIKA: Kabla sijamuita Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwita Getere swali la msingi lilitaja miradi hapa na naliona jibu limetaja miradi hiyo. Sasa ilipokuwa inaulizwa labda Mheshimiwa Naibu Waziri atatuambia sasa kama haiko Bunda hii miradi. Kwa sababu kama uliuliza kwa majina haya, na utakelezaji unaongelewa kuhusu majina ya miradi hii uliyoitaja, inawezekana iko Bunda lakini sio kwenye eneo lako. Sasa sijui uliulizaje wewe, kwa sababu swali lako linauliza kuhusu miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu ya hayo maswali mawili.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi tunaitekeleza kihalmashauri, hatutekelezi kijimbo, sasa hii ndiyo maana inawezekana katika programu ya huo mradi ilichukua vijiji vingi vya Jimbo lingine na vijiji vichache vikawa vya Jimbo la Mheshimiwa Getere, lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Getere kwamba utekelezaji unaendelea na mwaka huu tumeweka bajeti, kwa hiyo, tutaendelea ili kuhakikisha kwamba na vijiji vingi vilivyo sehemu ya kwako vinapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumzia kwamba kuna vijiji kama Nyamuswa ambavyo viko kilometa nne tu kutoka ziwani, ninaomba tushirikiane na Wilaya yako tuangalie kwamba ni kitu gani kitafanyika japo katika swali lako la pili umezungumzia fedha zilizotolewa kutoka kwenye hii programu ya *Lake Victoria Water and Sanitation Project* na mradi huo mkubwa unaendelea kuzunguka Ziwa letu la Victoria. Kwa hiyo, tutaangalia ni namna gani sasa tutaweza tukaweka mradi mwingine kupeleka maeneo haya ambayo umeyapendekeza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi tuko pamoja na tutahakikisha wananchi wako wanapata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Catherine Ruge.

Na. 498

Kupeleka Maji Mji wa Tarime kutoka Ziwa Victoria na Mto Mara

MHE. CATHERINE N. RUGE (K.n.y. MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Wilaya ya Tarime imepakana na Ziwa Victoria na Mto Mara ambao sehemu yake kubwa uko ndani ya Wilaya ya Tarime, licha ya kuwa karibu sana na vyanzo vya maji,

wananchi wa Tarime Mjini kwa muda mrefu wamekuwa wanatumia maji ya Bwawa la Kenya Manyori lililojengwa na Mjerumani ambalo halijawahi kufanyiwa usafi tangu kuchimbwa kwake na kupelekea wananchi watumie maji yasiyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ndani ya Mji wa Tarime kutoka Ziwa Victoria na Mto Mara kama ilivyowahi kuyapeleka Shinyanga?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta wataalam kusimamia na kuendeleza chanzo cha maji kilichopo japo hakikidhi mahitaji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Mji wa Tarime. Usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya mradi huo ulikamilika mwaka 2012 na kwa sasa Serikali inafanya mapitio ya usanifu wa mradi huo (*design review*) na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2017. Baada ya mapitio ya usanifu wa mradi kukamilika na gharama za ujenzi kufahamika, Wizara itatafuta fedha kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje, kadri hali itakavyoruhusu ili mradi uweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (*MUWASA*) imeandaa mradi wa kuboresha chanzo cha sasa cha Mto Nyandurumo ili kiweze kuzalisha maji mengi zaidi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya upanuzi wa choteo la maji (*water intake*) ili liweze kuingiza maji mengi zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa sawa ni milioni 500 au milioni 300?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni shilingi milioni 300.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherini Ruge swali la nyongeza.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ila napenda nikuambie Mheshimiwa Waziri ni asilimia chini ya 30 tu ya wakazi wa Mji wa Tarime wanaopata maji kutoka kwenye Bwawa la Nyanduruma na ambayo siyo safi na salama. Nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kuanzia Shirati kupitia Utegi, Ngiri Juu na kufikisha maji Sirali na Tarime, *design* ilimalizika mwaka 2011, lakini hapa kwenye jibu lako la msingi umesema *design review* itamalizika mwaka 2017. Lakini tunafahamu kwamba Benki ya Maendeleo ya Ufaransa, (*France Development Bank*) walikuwa tayari kufadhili mradi huu, ni nini sasa kinasababisha Serikali itafute mfadhili mwingine ili hali Benki ya Maendeleo ya Ufaransa iko tayari kufadhili mradi huu?

Swali la pili, kwa kuwa Mji wa Tarime ndiyo makao makuu ya Wilaya ya Tarime na ina taasisi mbalimbali kama hospitali, magereza, shule na kadhalika na ukosefu wa maji husababisha mlipuko wa magonjwa, ni lini sasa Serikali itachimba visima hasa kwenye taasisi hizi kama suluhisho la muda mfupi kwa kata zote za Mji wa Tarime?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa *review* ya mradi bado haijakamilika, hili ni suala la kitaalam unaweza ukalipata juu juu, lakini sisi tunasema *review* inakamilika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili amedai kwamba anataarifa sijui umezipata wapi, mimi ninafikiri taarifa unazipata za uhakika kutoka kwa sisi wenye Wizara, usipate taarifa za kutoka mtaani. Taarifa za kwetu za ndani ni kwamba bado hatujapata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huo mradi na kwa sababu hatujui ni kiasi gani kinahitajika, kwa ajili ya huo mradi. Kwa hiyo, tukishajua kiasi gani kitahitajika ndio sasa tutachukua hatua za kutafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kweli kwamba Tarime ni Makao Makuu ya Wilaya, lakini kwa kwa hatua za dharura Mheshimiwa Catherine ni kwamba tumechimba kisima kimoja tayari, tumekarabati visima viwili, tumeongeza mtandao wa kilometa 30 wa mabomba na ndiyo maana sasa tunaingia mkataba kwa ajili ya kuboresha chanzo cha Nyandurumo kama nilivyokuwa nimezungumza katika swali langu la msingi, lakini pia tutaendelea na kwa sababu tumetenga fedha niombe kwamba mwambie Mkurugenzi wako, aendelee kuweka mapendekezo kwa ajili ya kuongeza visima vingine ili maeneo ya mji, hospitali, taasisi za shule, ziweze kupata maji bila matatizo yoyote.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la dharura hapa.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Spika aliunda Kamati Maalum ya kushughulikia masuala ya Madini ya *Tanzanite* Wajumbe wa Kamati hii wanahitajika sasa hivi *Speaker's Lounge* yaani hapa nyuma, kwa hiyo, unaweza kupita upande huu utakuta mlango hapo nyuma, wanaitwa huko na Mwenyekiti wa Kamati hiyo maalum, Mheshimiwa Doto Biteko. Wanaitwa sasa hivi.

Baada ya tangazo hilo tutaendelea. Sasa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia sasa aulize swali lake.

Na. 499

Barabara ya Kilindoni – Rasi Mkumbi

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Ujenzi wa barabara kutoka Kilindoni – Mafia – Rasi Mkumbi kwa lami ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Ilani ya CCM 2015 – 2020.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kilindoni - Mafia hadi Rasi Mkumbi yenye urefu wa kilometa 51 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kilindoni - Mafia hadi Rasi Mkumbi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali inaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika katika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 359.52 kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya aina mbalimbali ya barabara hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau swali la yongeza.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru pia ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii sio ahadi tu ya Rais Mstaafu na kwenye Ilani ya Uchaguzi bali pia ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya ya Mafia mwezi Septemba, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mafia kwa kuwa ni kisiwa, hali ya upatikanaji wa udongo ni ndogo sana. Udongo unapatikana katika kijiji kimoja cha Bweni na wataalam wanasema baada ya miaka miwili udongo huo utakuwa umekwisha kabisa. Kwa hiyo, mtakapokuwa tayari kuja kujenga barabara ya lami, udongo Mafia utakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, sasa kwa kuwa Ilani ya CCM inasema mwaka huu mtaanza na usanifu na katika majibu yako hujasema hata kama usanifu utafanyika, swali la kwanza; kwa nini usanifu usifanyike mwaka huu ili ujenzi ufanyike mwakani?

La pili; ni kwanini sasa Serikali isitilie maanani hili suala la ukosefu wa udongo na kuharakisha ujenzi huu ifikapo mwakani? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpogezze sana Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau kwa namna anavyofuatilia masuala ya miundombinu katika Kisiwa cha Mafia na kwa kweli aliponipeleka Mafia mimi nimebadilika kabisa. Naomba nimhakikishie yale ambayo tuliyaongea tutayafuatilia ili kuhakikisha ahadi hii ambayo kama alivyosema sio ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne peke yake bali ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015; lakini

vilevile Waziri Mkuu alipokwenda pale ambapo yeye alitangulia kabla yangu naye alirudia kuahidi kutokana na mazingira yalivyo pale Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nikuhakikishie kwamba tutawasiliana ndani ya Wizara kama ambavyo tulikwambia awali ili tuone uwezekano wa kuanza *feasibility study and detailed design* ya barabara ile mwaka huu kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atatujaalia na mimi naamini Mwenyezi Mungu yupo upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dau kwa swali lako la pili naomba tukutane na Mheshimiwa Waziri wangu na kwa sababu leo ni siku ya mwisho ya Bunge na Waziri wangu yupo jana ulikutana nae lakini naomba tukutane nae tena ili tulikamilishe hili kama ambavyo uliambiwa na Waziri wangu jana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 500

Walimu Kupatiwa Mafunzo Maalum ya Kufundisha Wanafunzi Wenye Ulemavu

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

Kutokana na umuhimu wa elimu jumuishi Tanzania (*inclusive education*).

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kila mwalimu anapatiwa mafunzo maalum yatakayomuwezesha kufundisha wanafunzi wenye ulemavu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa mtaala mpya ambao umeandaliwa katika misingi ya elimu jumuishi na ulianza kutumika kuanzia mwaka wa masomo 2014/2015. Hadi sasa wahitimu wa ngazi ya Stashahada ya Elimu Maalum wapato 158 wamehitimu Oktoba, 2016 na wanachuo 248 wanaendelea na masomo katika Chuo cha Ualimu Patandi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhumu wa walimu hawa, Wizara katika mwaka wa fedha 2016/2017 iliendesha mafunzo kwa walimu kazini 519 wanaofundisha darasa la kwanza na la pil kuhusiana na mtaala ulioboreshwa ili kumudu ufundishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vilevile tarehe 20 mpaka 28 Juni, 2017 walimu kazini 712 wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wenye usonji walipatiwa mafunzo katika vituo vya Mwanza, Arusha, Mbeya na Morogoro ili kuwajengea uwezo wa kumudu ufundishaji wa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na usonji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, walimu 600 wanaofundisha darasa la tatu na la nne watapatiwa mafunzo ya mtaala ulioboreshwa kuanzia tarehe 10 hadi 30 Julai, 217 lengo ni kuwafikia walimu wengi zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stella Ikupa Alex swali la nyongeza.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba niendeele kutambua juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kupitia Wizara hii na hasa pale ilipotamka wazi kwenye hotuba yake kwamba imetoa kipaumbele cha elimu kwa watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea elimu jumishi tunamaanisha kwamba watoto wenye ulemavu wasome na wasio na ulemavu. Sasa Serikali inaonaje hii elimu maalum ikafundishwa kwenye vyuo vyote vya ualimu nchini tofauti na ilivyo sasa hivi kwamba ni walimu wachache wanaopata ujuzi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili katika hii mitaala mipya inayoandaliwa Serikali inaonaje ikaingiza lugha ya alama kuwa miongoni mwa masomo ambayo yatafundishwa ili kizazi kijacho kiweze kuwasiliana na viziwi kwa urahisi? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Ikupa kama ifuatavyo; ni kweli ili wanafunzi hawa waweze kupata haki yao ya msingi ya kuweza kujifunza vizuri popote walipo ni pale tutakapokuwa na walimu wa kutosha ambao wana uwezo wa kuwasiliana na kutoa elimu husika kwa watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni muhimu sana, lakini kwa sasa tunachoangalia ni kuona kwamba ni namna gani tunafanya hivyo, kwa mfano katika suala la lugha ya alama, Wizara tayari inaliangalia jambo hili ili kuwezesha walimu wote angalau wawe na msingi wa lugha ya alama ili kuweza kuwasaidia wanafunzi hao. Kwa hiyo, jambo hilo mimi naona tulichukue tuone ni namna gani tutalifanyia kazi. Kwa msingi huo nimejibu maswali yote mawili kwa pamoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tutamalizia na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ally Saleh Ally Mbunge wa Malindi swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Bobali.

Mheshimiwa Mbatia nilikuwa nimeletewa ujumbe hapa, kwa hiyo litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa James Mbatia.

Na. 501

Deni la Taifa

MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y MHE. ALLY SALEH ALLY)
aliuliza:-

Bunge lilipitisha Mpango wa Maendeleo na katika utekelezaji wake kasi ya Serikali kukopa imekuwa kubwa na bila shaka matokeo yake ni kuongezeka kwa Deni la Taifa:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili ni kiasi gani kimekopwa hadi sasa ndani na nje ya nchi?

(b) Je, Serikali inajipangaje kulipa deni hilo pamoja na deni ambalo tayari lipo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo (2016/2017 – 2020/2021) ulipitishwa na Bunge lako Tukufu na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwezi Juni, 2016. Serikali ilianza utekelezaji wa mpango huo mwezi Julai, 2017.

Katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji, Serikali ilitarajia kukopa jumla ya shilingi bilioni 9,653 kutoka katika soko la ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,374.30 zilitarajiwa kukopwa kutoka soko

la ndani shilingi bilioni 2,177.8 mikopo yenye masharti nafuu na shilingi bilioni 2,101.0 ni mikopo ya masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi 31, 2017, Serikali ilifanikiwa kukopa jumla ya shilingi bilioni 6,893.4 sawa na asilimia 71.4 ya lengo la kukopa shilingi bilioni 9,653.0. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 4,715.6 zilikopwa kutoka soko la ndani na shilingi bilioni 2,177.8 ni mikopo nafuu kutoka nje. Aidha, hatukuweza kukopa kutoka katika chanzo cha masharti ya kibiashara katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizi napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa, si kweli kwamba tangu tupitische Mpango wa Maendeleo Juni, 2016 kasi ya kuongezeka kwa Deni la Taifa imekuwa kubwa. Hata hivyo, hatuwezi kupima kasi ya ongezeko la Deni la Taifa ndani ya mwaka mmoja wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, madeni yote ya Serikali yakijumuisha mtaji pamoja na riba yanalipwa kupitia mfumo wa kawaida wa bajeti ya Serikali. Katika mwaka 2016/2017, Serikali ilitenga shilingi bilioni 4,866.3 kwa ajili ya kulipa mtaji na riba ya deni la ndani na shilingi bilioni 1,586.6 kwa ajili ya kulipa mtaji na riba ya deni la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi 31,2017, shilingi bilioni 3,657.74 zilitumika kulipa mtaji wa deni la ndani, shilingi bilioni 796.16 zilitumika kulipa riba ya deni la ndani, shilingi bilioni 766.02 zilitumika kulipa mtaji wa deni la nje na shilingi bilioni 436.56 zilitumika kulipa riba ya deni la nje. Hadi sasa Serikali inahudumia au kulipa deni lake (ndani na nje) kwa mujibu wa masharti ya mikopo husika na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 7,830.0 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali litakaloiva kati ya Julai, 2017 na Juni 2018. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,973.8 zimetengwa kwa ajili ya deni la ndani na shilingi bilioni 1,856.1 ni kwa ajili ya deni la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, kutafuta mikopo nafuu na kukopa mikopo michache ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye kuchochea kwa haraka ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na hivyo kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linaendelea kuhudumiwa kwa wakati na kwa mujibu wa masharti, sheria, kanuni na taratibu za mikopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa James Mbatia, swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi lilikuwa linauliza kiasi cha Deni la Taifa hadi sasa. Mheshimiwa Waziri hakujiibu kabisa hilo ndiyo swali limeulizwa lakini hakulijibu hilo kabisa! Amekuja na mambo mengine mengi tu.

Kwa kuwa yote aliyosema Mheshimiwa Waziri katika kujibu swali hili ameonesha kwamba mwaka huu wa fedha 2017/2018 Serikali imejipanga kukopa shilingi trilioni 8.83 ambapo wastani kwa mwezi ni sawa na kukopa shilingi bilioni 652 na mishahara ni takribani shilingi bilioni 600. Kwa hivyo kwa mwezi tutakuwa tunalipa mishahara pamoja na kulipa Deni la Taifa. Je, fedha za maendeleo zitapatikana wapi kama tutakuwa tunalipia tu Deni la Taifa pamoja na mishahara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoingia madarakani Deni la Taifa lilikuwa ni shilingi trilioni 35 lakini hadi mwezi Machi mwaka huu deni la Taifa limeongezeka na kufika shilingi trilioni 50.8 kwa kasi kubwa namna hii ya kukopa tunalipeleka wapi Taifa letu ambapo tutaweza tukaangamia? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuliambia Bunge lako tukufu swali kama lilivyolizwa ndivyo nilivyolijibu kwa sababu limeulizwa tangu tumepitisha Mpango wa Maendeleo. Mpango wa Maendeleo tunautekeleza sasa ni mpango tulioupitisha mwaka 2016/2017 na ndio tunautekeleza na ndivyo tulivyojibu swali letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha za maendeleo; upatikanaji wa fedha za maendeleo unapatikana kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tunaimarisha ukusanyaji wa mapato, kwa hiyo, tunaweza kulipa deni letu na deni letu la ndani inakuwa ni *rollover*.

Kwa hiyo, hiki alichokisema Mheshimiwa James Mbatia inawezekana kabisa kwa sababu hii ni *rollover* tuna *roll* mikopo yetu tunaweza kulipa riba yetu na tunaweza kulipa deni letu la nje. Kwa hiyo, tuna uwezo wa kulipa deni letu na tuna uwezo wa kuendelea kutekeleza miradi yetu ya maendeleo kama tulivyofanya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza tunalipeleka wapi Taifa letu.

Napenda kurejea kauli yangu niliyoisema ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba *what matters is not how much you have borrowed but for what have you borrowed*; tunakopa ili kutekeleza miradi ya maendeleo, miradi ya kimkakati, miradi inayochochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na hakuna duniani hata Marekani yenyewe inakopa na inaweza kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiangalia uchumi wa Taifa letu unakuwaje, miundombinu ya Taifa letu inayopelekea ukuaji wa uchumi wetu inatekelezwa kwa kiasi gani. Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo mezani leo na tunayo matangazo ya wageni na tutaanza na wageni ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba ambaye ni Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na hawa ni wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kutoka *Mzizima Savings and Credit Cooperative Union (MSAKU)*. Popote walipo wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 30 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Wabunge wengine wa Singida ambao ni viongozi pamoja na wachezaji wa timu ya *Singida United Football Club* kutoka mkoani Singida. Hawa wameongozana na kocha wao mkuu, kocha Hans Van De Pluijim. Waheshimiwa Wabunge, hii timu Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kuwa kocha wake, kwa hiyo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 54 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni wanafunzi 49 wa darasa la saba na wanafunzi watano wa shule ya msingi Tumaini iliyopo Kata ya Nkuhungu, Wilaya ya Dodoma Mjini Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni pia waliotutembelea kwa ajili ya kujifunza na hawa ni wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba Muhimbili kutoka Jijini Dar es Salaam na wako Mkoani Dodoma kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika Hospitali ya Mirembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayotutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu

NDG.LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali ya mwaka 2017 (*The Written Laws
(Miscellaneous Amendments Bill) Act, 2017*)**

(Kusomwa Mara Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nitamuita Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze kuwasilisha Muswada huo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*) kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitisha Muswada huu kuwa sehemu ya sheria ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Ninawashauri Watanzania wote tuendeleo kumuunga mkono na pia kumuomba kwa Mwenyezi Mungu.

Pia ninawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais, wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Mawaziri kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nikiwapongeza jinsi walivyoleta hotuba muhimu za bajeti za Wizara zao na kupitishwa na Bunge. Miongoni mwao nimtaje tu hapa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi kwa ushirikiano mkubwa anaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi kwa kuweza kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Miswada mitatu muhimu kwa maslahi ya Taifa letu ambayo ni *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017*, *The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017* na *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*. Miswada hiyo tayari imepitishwa na Bunge kuwa sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalishukuru Bunge kwa kutambua umuhimu wa Miswada hiyo na kuipitisha kuwa miongoni mwa sheria za nchi yetu. Hakika wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu mnaingia katika historia muhimu kuhusu kutungwa kwa sheria hizo zinazohusu umiliki na matumizi bora ya maliasili na rasilimali za nchi yetu kwa manufaa ya wananchi na nchi yetu ipasavyo. Ninawashauri wananchi kuchangamkia na kufaidika na fursa zinazoletwa na sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendelea kuliongoza

Bunge letu kwa ufanisi ipasavyo. Pia ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge na Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Salma Rashid, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Ninawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya Bunge hili na pia katika kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu Gerson Mdemu, kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali kwa ufanisi ipasavyo licha ya changamoto mbalimbali.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivyo kutupatia kwa njia ya ushauri, maombi, sala, dua, taarifa muhimu na kadhalika na hivyo kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapowasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu, ninatambua kwamba Taifa limepitia katika vipindi mbalimbali vya maombi na toba kuanzia Kwaresma, Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ibada za kila juma au kila siku. Wabunge ni miongoni mwa wananchi ambao wamekuwa wakishiriki ibada hizo na hata wakati mwingine katika maeneo haya ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hatua hii ya wananchi kushiriki ibada hizo italiwezesha Taifa letu kubarikiwa na kudumisha amani, mshikamano, umoja na

ustawi wa wananchi. Kwa hiyo, ninawapongeza sana wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushiriki katika ibada hizo, Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki, Mwenyezi Mungu ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge wa Rufiji) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*) unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati kutumia masharti ya sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya Sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyoko katika sheria nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kubadilisha vifungu vya Sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na

kuiandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazopendekezwa kurekebisha kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (*The Budget Act, [Cap.439]*), na pili Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268 (*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, [Cap. 268]*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambapo sehemu ya kwanza ya muswada inaainisha masharti ya utangulizi, ikiwa ni pamoja na, jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura 439 (*The Budget Act, Cap 349*). Kwa ujumla msingi wa marekebisho yanayopendekezwa ni changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza Sheria ya Bajeti kama ilivyo hivi sasa. Sheria hiyo kwa sasa inaweka masharti yanayoitaka Serikali kuwasilisha Bungeni kila robo mwaka taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Utaratibu huo hautoi fursa ya kutosha kwa Serikali kuandaa taarifa husika na kufanya mapitio ya kina ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Utekelezaji wa bajeti ya Serikali, pamoja na mambo mengine, unategemea kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi na mapato hayo ya kila mwezi ndiyo

yanayotolewa kwa mafungu mbalimbali ili kutekeleza bajeti ya Serikali. Kila ifikapo robo ya mwaka, Serikali inakuwa haijapokea mapato ya kutosha kutoka vyanzo vyake ikiwemo kutoka kwa washirika wa maendeleo na hivyo taarifa husika kukosa uhalisia.

(ii) Ili kuandaa ipasavyo taarifa za utekelezaji wa bajeti, Wizara na Taasisi mbalimbali zinahitaji muda wa kutosha wa kukusanya takwimu, kuzifanyia uchambuzi na hatimaye kuandaa taarifa husika na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi na kuzijumuisha pamoja (*consolidate*). Muda wa robo mwaka uliopo hivi sasa kisheria hautoi fursa kwa Taasisi na Wizara kukusanya takwimu sahihi na kuzifanyia uchambuzi ili kuandaa taarifa zenye kubainisha hali halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo, Muswada huu unapendekeza marekebisho katika sheria hiyo ili kuweka masharti yatakayowezesha taarifa mbalimbali kuhusiana na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kuwasilishwa Bungeni kila nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo itawezesha Serikali kupata fursa ya kutosha ya kuandaa taarifa inayojitoseheza kuhusiana na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali baada ya kupata mapato na matumizi na hivyo kuweza kuandaa takwimu muhimu kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 41(7) cha sheria hiyo kinachohusiana na uhamisho wa fedha (*reallocation*) na uwasilishaji wa taarifa za uhamisho huo Bungeni. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa uhamisho wa fedha ufanywe na Waziri mwenye dhamana ya fedha na kwamba taarifa ya uhamisho wa fedha iwasilishwe Bungeni kila robo mwaka (*quarterly*).

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayopendekezwa kupitia Muswada huu ni kuweka masharti katika kifungu kipyua 41(8) kuwa taarifa za uhamisho wa fedha iwasilishwe Bungeni kila baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 53(2) cha sheria kinachoweka masharti kwamba Waziri mwenye dhamana ya fedha awasilishe Bungeni taarifa ya robo mwaka kuhusu miadi ya matumizi ya kila kasma (*Report Expenditure Commitment*). Muswada unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe ili taarifa ya robo mwaka kuhusu miadi ya matumizi ziwasilishwe Bungeni kila baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 56(1) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha awasilishe Bungeni taarifa ya utekelezaji wa bajeti (*compliance report*) ya Serikali kila baada ya robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kuweka masharti yatakayowezesha taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuwasilishwa Bungeni miezi sita baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali na kila mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Muswada unapendekeza kifungu kidogo cha (7) kifutwe kwa kuwa maudhui yake tayari yameelezwa katika kifungu kidogo kipyua cha (1) kinachopendekezwa kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 57 cha Sheria ya Bajeti kinaweka masharti kuhusu taarifa ya robo mwaka

ya mapato na matumizi halisi ya Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma (*Quarterly Statements of the Government*). Marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 7 ya Muswada ni kufanya marekebisho ya kiuandishi katika maelezo ya pembeni "*marginal note*" kwa kufuta maneno "*Quarterly statements*" na kuweka badala yake maneno "*Mid year statements*."

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inapendekezwa kuwa kifungu cha kidogo cha (1) kifutwe na kuandikwa upya ili taarifa ya mapato na matumizi halisi ya Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma iwasilishwe Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya fedha miezi sita baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali badala ya kila robo mwaka kama inavyoelezwa katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 61 cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha anaweza kusamehe kodi, ada na tozo mbalimbali na kwamba awasilishe Bungeni taarifa ya misamaha kila robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu hicho ili kuweka masharti kuwa taarifa ya misamaha hiyo iwasilishwe Bungeni kila nusu mwaka badala ya muda wa robo mwaka unaotajwa katika Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 62(2)(a) kwa kufuta neno "*port folio*" na kuliandika kwa usahihi kuwa "*portfolio*."

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 63(2)(b) kinachohusu

uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali Bungeni kila baada ya robo mwaka, kwa kufuta neno “*quarterly*” na kuweka badala yake neno “*mid-year.*” Lengo la mapendekezo haya ni kuweka masharti yatakawezesha taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kila baada ya nusu mwaka kama iliyopendekezwa pia katika Ibara ya 6 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 65(2) cha Sheria ya Bajeti kinaweka masharti kuwa iwapo itathibitika kuwa Afisa wa Umma kwa makusudi au kutokana na uzembe alisababisha Serikali au Taasisi ya Umma kushindwa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hiyo anatenda kosa la kinidhamu (*disciplinary offence*) na atawajibishwa binafsi kwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kushtakiwa kwa kosa la jinai kulingana na aina (*nature*) ya madhara yatokanayo na kushindwa kutekeleza majukumu hayo, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa maafisa husika wanatekeleza ipasavyo masharti ya Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali(Utekelezaji wa Majukumu) Sura ya 268 (*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, [Cap.268]*). Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8(2) cha sheria hiyo kwa kufuta neno “*ordinance*” popote linapojitokeza katika kifungu hicho na kuweka badala yake neno “*Act*” kwa kuwa hilo ndilo neno sahihi linalotumika kutaja sheria ikiwemo sheria zinazorejewa katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inapendekezwa kuwa rejea ya Sheria ya Uasili (*Adoption*) ifutwe na kuweka badala yake rejea ya Sheria ya Mtoto (*The Law of the Child*). Hii ni kwa sababu Sheria ya *The Adoption Ordinance* ilishafutwa kupitia Sheria ya Mtoto ambayo ndiyo inayosimamia masuala ya kuasili mtoto kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufuta kichwa cha Sehemu ya Saba katika sheria hiyo ili kisomeke *“Recruitment and Code of Ethics for Law Officers, State Attorneys and Legal Officers”* badala ya *“Recruitment and Code of Ethics for Legal Officers.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu masharti kuhusu ajira na Kanuni za Maadili ambayo yako katika vifungu vya 24 hadi 29 vya sehemu hiyo yanawahusu pia *“Law Officers”* na *“State Attorneys”* kama inavyoonekana pia katika Jedwali la Sheria hiyo na siyo *“Legal Officers”* pekee kama inavyoelezwa katika kichwa cha sehemu hiyo ya saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 cha Sheria hiyo kinampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kusikilizwa katika mashauri yenye maslahi ya umma mahakamani, mabarazani na katika taasisi za kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kifungu 17(1) kwa jinsi kilivyoandikwa hakieleweki vizuri kisarufi na kimaudhui na pia kinaonekana kama kimejikita tu katika mashauri yaliyoko katika ya *administrative body* pekee wakati masharti mengine ya kifungu hicho yanahusisha pia mashauri yaliyoko mahakamani na mabarazani yenye maslahi ya umma, mali ya umma au mashauri ambayo yanahusu Bunge, Mahakama, Idara inayojitegemea ya Serikali au Wakala ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa kuzingatia pia kuwa Ibara ya 59(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Katiba) inampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali “haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano” na kwa kuwa shauri katika mahakama hizo linaweza kufunguliwa kwa njia ya mbali mbali ikiwemo *“application,” “suit” au “petition,”*

Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kufuta maneno “*suit inquiry on administrative body*” katika kifungu hicho na kuweka badala yake maneno “*application, suit, appeal or petition in court or inquiry on administrative body.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa marekebisho haya ni kuwezesha Ibara ya 59(4) ya Katiba kutekelezwa kwa ufanisi ipasavyo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kusikilizwa katika shauri lolote lililofunguliwa au linaloendelea mahakamani katika Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi au mali ya umma na kushiriki katika mashauri yanayohusu Bunge, Mahakama, Idara inayojitegema au Wakala ya Serikali katika shauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*) na ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**HOTUBA YA NDUGU GEORGE M. MASAJU, MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2017
(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT,
2017) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa Hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2016 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017**) kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebishosasa usomwe Mara ya Pili; na Bunge lako Tukufu Ijadili na hatimaye lipitisha Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017**).

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu.

Ninawashauri Watanzania wote tuendeleo kumuunga mkono na pia kumuomba kwa Mwenyezi Mungu. Pia, ninawapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt. Ally Mohamed Shein Rais, wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Kassim Majaliwa, Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea

maendeleo Watanzania wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ninawashukuru Mawaziri kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake huku nikiwapongeza jinsi walivyoleta hotuba muhimu za bajeti za Wizara zao na kupitishwa na Bunge. Miongoni mwao nimtaje tu hapa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe Prof. Palamagamba John Kabudi (Mb) kwa ushirikiano mkubwa anaopatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ninampongeza Mhe Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) kwa kuweza kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Miswada mitatu muhimu kwa maslahi ya Taifa letu ambayo ni **The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017, The Natural Wealth and Resources (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017** na **The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017** . Miswada hiyo tayari imepitishwa na Bunge kuwa Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ninalishukuru Bunge kwa kutambua umuhimu wa Miswada hiyo na kuipitisha kuwa miongoni mwa sheria za Nchi yetu. Hakika wewe mwenyewe Mhe. Spika na Bunge lako Tukufu mnaingia katika historia muhimu kuhusu kutungwa kwa Sheria hizo zinazohusu umiliki na matumizi bora ya Maliasili na Rasilimali za Nchi yetu kwa manufaa ya Wananchi na Nchi yetu ipasavyo. Ninawashauri wananchi kuchangamkia na kufaidika na fursa zinazoletwa na Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa

Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendelea kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi ipasavyo. Pia, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mhe. Salma Rashid Kikwete (Mb.), Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare(Mb.) na Mhe. Catherine Nyakao Ruge (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Ninawatakiwa kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya Bunge hili na pia katika kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninawapongezawatumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu Gerson J. Mdemu, kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali kwa ufanisi ipasavyo licha ya changamoto mbalimbali. Mwisho,lakini sio kwa umuhimu, ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Ofisi ya Mwasheria Mkuu wa Serikali na hivyo kutupatia kwa njia ya ushauri, Maombi, Sala, Dua, taarifa muhimu n.k. na hivyo kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ninapowasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako tukufu, ninatambua kwamba Taifa limepitia katika vipindi mbalimbali vya maombi na toba kuanzia Kwaresma, Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ibada za kila juma au kila siku. Wabunge ni miongoni mwa Wananchi ambao wamekuwa wakishiriki ibada hizo na hata wakati mwingine katika maeneo haya ya Bunge. Ninaamini kwamba hatua hii ya wananchi kushiriki ibada hizo italiwezesha Taifa letu kubarikiwa na kudumisha amani,

mshikamano, umoja na ustawi wa wananchi. Kwa hiyo ninawapongeza sana wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushiriki katika ibada hizo, Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki, Mwenyezi Mungu ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amina.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017**) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge wa Rufiji) na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017, (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017**), unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Mbili (2). Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati kutumia masharti ya sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya Sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyoko katika sheria nyingine zilizopo. Baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika Muswada huu, ni kubadilisha vifungu vya Sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

1. Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (**The Budget Act, [Cap.439]**); na

2. Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali(Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268(**The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, [Cap. 268]**);

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya Utangulizi, ikiwa ni pamoja na, jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura 439 (**The Budget Act, Cap 349**). Kwa ujumla, msingiwa marekebisho yanayopendekezwa ni changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza Sheria ya Bajeti kama ilivyo hivi sasa. Sheria hiyo kwa sasa inaweka masharti yanayoitaka Serikali kuwasilisha Bungeni kila robo mwaka taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Utaratibu huo hautoi fursa ya kutosha kwa Serikali kuandaa taarifa husika na kufanya mapitio ya kina ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kutokana na sababu zifuatazo;

(i) Utekelezaji wa bajeti ya Serikali, pamoja na mambo mengine, unategemea kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi na mapato hayo ya kila mwezi ndiyo yanayotolewa kwa mafungu mbalimbali ili kutekeleza bajeti ya Serikali. Kila ifikapo robo ya mwaka, Serikali inakuwa haijapokea mapato ya kutosha kutoka vyanzo vyake

ikiwemo kutoka kwa washirika wa maendeleo na hivyo taarifa husika kukosa uhalisia.

(ii) Ili kuandaa ipasavyo taarifa za utekelezaji wa bajeti, Wizara na Taasisi mbalimbali zinahitaji muda wa kutosha wa kukusanya takwimu, kuzifanyia uchambuzi na hatimaye kuandaa taarifa husika na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi na kuzijumuisha pamoja (*consolidate*). Muda wa robo mwaka uliopo hivi sasa kisheria hautoi fursa kwa Taasisi na Wizara kukusanya takwimu sahihi na kuzifanyia uchambuzi ili kuandaa taarifa zenye kubainisha hali halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria hiyo ili kuweka masharti yatakayowezesha taarifa mbali mbali kuhusiana na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kuwasilishwa Bungeni kila nusu mwaka. Hatua hiyo itawezesha Serikali kupata fursa ya kutosha ya kuandaa taarifa inayojitosheleza kuhusiana na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali baada ya kupata mapato na matumizi na hivyo kuweza kuandaa takwimu muhimu kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 41(7) cha Sheria hiyo kinachohusiana na uhamisho wa fedha (*reallocation*) na uwasilishaji wa taarifa za uhamisho huoBungeni.

Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa uhamisho wa fedha ufanywe na Waziri mwenye dhamana ya fedha na kwamba taarifa ya uhamisho wa fedha iwasilishwe Bungeni kila robo mwaka (*quarterly*). Marekebisho yanayopendekezwa kupitia Muswada huu ni kuweka masharti katika kifungu kipya 41(8) kuwa taarifa za uhamisho wa fedha iwasilishwe Bungeni kila baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 53(2) cha Sheria kinachoweka masharti kwamba Waziri mwenye dhamana ya fedha awasilishe Bungeni taarifa ya robo mwaka kuhusu miadi ya matumizi ya kila kasma (*report expenditure commitment*). Muswada unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe ili taarifa ya robo mwaka kuhusu miadi ya matumizi ziwasilishwe Bungeni kila baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 56(1) cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha awasilishe Bungeni taarifa ya utekelezaji wa bajeti (*compliance report*) ya Serikali kila baada ya robo mwaka. Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kuweka masharti yatakayowezesha taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuwasilishwa Bungeni miezi sita baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali na kila mwisho wa mwaka wa fedha. Pia, Muswada unapendekeza kifungu kidogo cha (7) kifutwe kwa kuwa maudhui yake tayari yameelezwa katika kifungu kidogo kipya cha (1) kinachopendekezwa kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 57 cha Sheria ya Bajeti kinaweka masharti kuhusu taarifa ya robo mwaka ya mapato na matumizi halisi ya Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma (*Quarterly Statements of the Government*). Marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 7 ya Muswada ni kufanya marekebisho ya kiuandishi katika maelezo ya pembeni "*Marginal Note*" kwa kufuta maneno "*Quarterly statements*" na kuweka badala yake maneno "*Mid year statements*". Pia, inapendekezwa kuwa kifungu cha kidogo cha (1) kifutwe na kuandikwa upya ili taarifa ya mapato na matumizi halisi ya Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma iwasilishwe Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya fedha miezi sita baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali badala ya kila robo mwaka kama inavyoelezwa katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 61 cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha anaweza kusamehe kodi, ada na tozo mbalimbali na kwamba awasilishe Bungeni taarifa ya misamaha kila robo mwaka. Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu hicho ili kuweka masharti kuwa taarifa ya misamaha hiyo iwasilishwe Bungeni kila nusu mwaka badala ya muda wa robo mwaka unaotajwa katika Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 62 kifungu kidogo cha (2)(a) kwa kufuta neno "*port folio*" na kuliandika kwa usahihi kuwa "*portfolio*".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 63(2)(b) kinachohusu uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali Bungeni kila baada ya robo mwaka, kwa kufuta neno "*quarterly*" na kuweka badala yake neno "*mid-year*". Lengo la mapendekezo haya ni kuweka masharti yatakayoweza taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kila baada ya nusu mwaka kama iliyopendekezwa pia katika Ibara ya 6 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 65(2) cha Sheria ya Bajeti kinaweka masharti kuwa iwapo itathibitika kuwa afisa wa umma kwa maksudi au kutokana na uzembe alisababisha Serikali au Taasisi ya Umma kushindwa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hiyo anatenda kosa la kinidhamu (*disciplinary offence*) na atawajibishwa binafsi kwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu aukushtakiwa kwa kosa la jinai kulingana na aina (nature) ya madhara yatokanayo na kushindwa kutekeleza majukumu hayo, kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa maafisa husika wanatekeleza ipasavyo masharti ya Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali(Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268(**The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, [Cap. 268]**). Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8(2) cha Sheria hiyo kwa kufuta neno "*Ordinance*" popote linapojitokeza katika kifungu hicho na kuweka badala yake neno "*Act*" kwa kuwa hilo ndilo neno sahihi linalotumika kutaja Sheria ikiwemo Sheria zinazorejewa katika kifungu hicho.

Pia, inapendekezwa kuwa rejea ya Sheria ya Uasili (*Adoption*) ifutwe na kuweka badala yake rejea ya Sheria ya Mtoto (*The Law of the Child*). Hii ni kwa sababu Sheria ya *The Adoption Ordinance* ilishafutwa kupitia Sheria ya Mtoto ambayo ndiyo inayosimamia masuala ya kuasili mtoto kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufuta kichwa cha Sehemu ya Saba katika Sheria hiyo ili kisomeke "*Recruitment and Code of Ethics for Law Officers, State Attorneys and Legal Officers*" badala ya "*Recruitment and Code of Ethics for Legal Officers*". Hii ni kwa sababu masharti kuhusu ajira na Kanuni za Maadili ambayo yako katika vifungu vya 24 hadi 29 vya Sehemu hiyo yanawahusu pia "*Law Officers*" na "*State Attorneys*" kama inavyoonekana pia katika Jedwali la Sheria hiyo na siyo "*legal officers*" pekee kama inavyoelezwa katika kichwa cha Sehemu hiyo ya Saba.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 cha Sheria hiyo kinampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kusikilizwa katika mashauri yenye maslahi ya Umma Mahakamani, Mabarazani na katika Taasisi za Kiutawala. Lakini Kifungu 17(1) kwa jinsi kilivyoandikwa hakieleweki vizuri kisarufi na kimaudhui na pia kinaonekana kama kimejikita tu katika mashauri yaliyoko katika ya *administrative body* pekee wakati masharti mengine ya kifungu hicho yanahusisha pia mashauri

yaliyoko Mahakamani na Mabarazani yenye maslahi ya umma, mali ya umma au mashauri ambayo yanahusu Bunge, Mahakama, Idara inayojitegema ya Serikali au Wakala ya Serikali.

Hivyo, kwa kuzingatia pia kuwa Ibara ya 59(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Katiba) inampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali "haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano" na kwa kuwa shauri katika Mahakama hizo linaweza kufunguliwa kwa njia ya mbali mbali ikiwemo "*application*", "*suit*" au "*petition*", Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kufuta maneno "*suit inquiry on administrative body*" katika kifungu hicho na kuweka badala yake maneno "*application, suit, appeal or petition in court or inquiry on administrative body*".

Msingi wa marekebisho haya ni kuwezesha Ibara ya 59(4) ya Katiba kutekelezwa kwa ufanisi ipasavyo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kusikilizwa katika shauri lolote lililofunguliwa au linaloendelea Mahakamani katika Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi au mali ya Umma na kushiriki katika mashauri yanayohusu Bunge, Mahakama, Idara inayojitegema au Wakala ya Serikali katika shauri husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017**) na ninaomba Bunge lako tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
SPECIAL BILL SUPPLEMENT

No. 1

12th January, 2017

to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.1 Vol.98 dated 12th January, 2017
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
11 January, 2017
Cabinet

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the

A Bill
for

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

- Short title **1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017.
- Amendment of certain written laws **2.** The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

AMENDMENT OF THE BUDGET ACT
(CAP.439)

- Construction Cap. 439 **3.** This Part shall be read as one with the Budget Act, hereinafter referred to as the "principal Act".
- Amendment of section 41 **4.** The principal Act is amended in section 41, by deleting subsection (7) and substitution for it the following:
 “(7) Any reallocations of funds shall be made in consultation with affected Government Ministries and government entities.
 (8) The Minister shall lay before the National Assembly a mid-year report in respect of reallocation made under this section.”
- Amendment of section 53 **5.** The principal Act is amended in subsection (2) of section 53, by deleting the words "every quarter" appearing in the second line and substituting for them the words "mid-year".
- Amendment of section 56 **6.** The principal Act is amended in section 56, by-
(a) deleting subsection (1) and substituting for it

the following:

“(1) The Minister shall, six months after approval of the annual national budget by the National Assembly and at the end of each financial year, lay before the National Assembly a compliance report.”

(b) deleting subsection (7).

Amendment of section 57

7. The principal Act is amended in section 57, by-

(a) deleting the words “Quarterly statements” appearing in the marginal note and substituting for them the words “Mid-year Statement”; and

(b) deleting subsection (1) and substituting for it the following:

“(1) The Accountant-General shall prepare the aggregate actual revenue and expenditure of the Government and public entities and forward to Minister who shall, six months after approval of annual national budget, submit the same to the National Assembly.”.

Repeal of section 61

8. The principal Act is amended by repealing section 61 and replacing for it the following:

“Powers of the Minister to waive tax, fees or charges
61. The Minister may waive tax, fees or charge imposed by the Government in accordance with criteria provided for under any written law, provided that he maintains a record of each waiver together with the reasons for the waiver and submit a mid-year report to the National Assembly.”.

Amendme
nt of
section 62

9. The principal Act is amended in section 62, by deleting the words "port folio" appearing in paragraph (a) of subsection (2) and substituting for them the word "portfolio".

Amendme
nt of
section 63

10. The principal Act is amended in section 63, by deleting the word "quarterly" appearing in paragraph (b) of subsection (2) and substituting for it the words "mid-year".

Amendme
nt of
section 65

11. The principal Act is amended in subsection (2) of section 65, by deleting the words "held personally liable for a disciplinary penalty" and substituting for them the words "subject to a deduction of six months' salary and other disciplinary measures in accordance with the Public Service Act".

Cap 298

PART III
AMENDMENT OF THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL
(DISCHARGE OF DUTIES) ACT
(CAP.268)

Constructio
n
Cap.268

11. This Part shall be read as one with the Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, hereinafter referred to as the principal Act".

Amendme
nt of
section 8

12. The principal Act is amended in subsection (2) of section 8 by:
(a) deleting the term "Ordinance" wherever it appears in that subsection and substituting for it the term "Act"; and

(b)in paragraph (b), deleting the term “Adoption” and substituting for it the term “Law of the Child”.

Amendme
nt of the
Heading of
Part VII

13. The principal Act is amended by deleting the “heading of Part VII” and substituting for it the following:

“RECRUITMENT AND CODE OF ETHICS FOR LAW OFFICERS, STATE ATTORNEYS AND LEGAL OFFICERS”

Amendme
nt of
section 17

14. The principal Act is amended in subsection (1) of section 17 by deleting the phrase “suit inquiry on administrative body” and substituting for it the words “application, suit or petition in court, or inquiry on administrative body”.

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend certain written laws, namely the Budget Act, Cap.439 and the Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap.268. The proposed amendments intend to update the respective laws with changes so far observed in their implementation.

This Bill is divided into Three Parts. Part I deals with Preliminary Provisions which includes the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.

Part II proposes amendments to the Budget Act, Cap.439. It is proposed to amend sections 41(7), 53(2), 56(1) and (7), 57, 61, 62 and 63 to enable the Government to submit reallocations reports, expenditure commitments reports, compliance reports, revenue and expenditure statements of the Government and tax waiver reports in every six months instead of quarterly basis as provided for under the Act. The amendments aim at providing sufficient time for the Government to collect and scrutinize information before finalization of such reports and its submission to the National Assembly.

It also proposed to amend section 65(2) so as to increase penalties for public officers who contravenes the provisions of the Act.

Part III proposes amendments to the Office of the Attorney General (Discharge of Duties), Cap.268. The proposed amendments intend to delete the term "Ordinance" wherever it appears in subsection (2) of sections 8 and substituting for it the term "Act". Further, it is proposed to delete the term "Adoption" appearing in paragraph (b) of subsection (2) and substituting for it the term "Law of the Child". The proposed amendment intends to update the Act with amendments made in 2002 and 2009, thus replacing the "Ordinances" with "Acts", and the "Adoption Ordinance" with the "Law of the Child". Further, it is proposed to delete the heading of Part VII and substituting for it a new heading. Furthermore, it is proposed to amend subsection (1) of section 17 in order to correct typographic errors and bring clarity to that subsection.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268. Marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kurekebisha zitakavyorekebisha ndani ya Muswada huu.

Shemu ya Pili inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Marekebisho yanapendekezwa katika vifungu vya 41(7), 53(2), 56(1) na (7), 57, 61, 62 na 63 kwa lengo la kuiwezesha Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa za uhamisho wa fedha, taarifa za matumizi, taarifa za utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha ya kodi mbalimbali na taarifa za mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ilivyoainishwa kwenye vifungu tajwa.

Marekebisho haya yanalenga kuipatia Serikali muda wa kutosha kukusanya na kupitia taarifa hizo kabla ya kuziwasilisha Bungeni.

Aidha, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 65(2) kwa lengo la kuongeza adhabu kwa maafisa wa umma watakaokiuka masharti ya Sheria hii.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268. Marekebisho hayo yanapendekezwa katika vifungu vya 8, kichwa cha Sehemu ya Saba na kifungu cha 17(1) ambayo yanaondoa mapungufu ya kiuandishi. Dhamira ni kwenda sambamba na marekebisho yaliyofanywa mwaka 2002 na 2009. Marekebisho hayo yaliondoa neno "Ordinance" na kuweka neno "Act". Aidha, yalifuta Sheria ya Uasili na badala yake kutunga Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Vile vile, inapendekezwa kufanya marekebisho ya kiuhariri katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 17.

Dar es Salaam,
10 Januari, 2017

GEORGE M. MASAJU
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

NAIBU SPIKA: Tutaendelea na kumsikiliza Mwenyekiti wa kamati ya Katiba na Sheria.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, (Na. 1) wa mwaka 2017 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, No. 1 of 2017*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 wa mwaka 2017 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.1) Act of 2017*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo ni kikao cha mwisho cha Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Moja, kabla sijaingia katika masuala ya msingi ya Muswada huu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, na kukupongeza wewe kwa dhati Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia kwa umahiri shughuli zote za Bunge hili la Kumi na Moja.

Bunge hili sasa limeingia katika historia hasa kwa kupitisha miswada miwili ya Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill*) na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za nchi wa mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*) pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hizi zote zinawakilisha Tanzania mpya. Hongera sana Mheshimiwa Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kufanikisha suala hili katika Bunge lako tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu mwezi Januari, 2017 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Sita wa Bunge ili ufanyiwe kazi na mnamo tarehe 7 Machi, 2017, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango walifika mbele ya Kamati yangu iliyoketi hapa Dodoma na kutoa maelezo kuhusu malengo na madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za msingi katika sheria husika kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Fedha na Mipango kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo ya kina kuhusu sababu za Serikali kupendekeza marekebisho haya ya sheria, majadiliano ya kina kati ya Serikali, Kamati za Bunge na taasisi nyingine yaliendelea kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Januari tarehe 4 Julai, 2017 Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango walifika kwa mara nyingine tena mbele ya Kamati yangu ili kutoa majibu ya hoja za Kamati na wadau mbalimbali kutokana na vikao vya kujadili mapendekezo ya marekebisho haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni matokeo muafaka uliofikiwa kati ya Kamati na Serikali kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuanzia mwaka huu wa fedha 2017/2018 ambao utaleta tija katika utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015; Sura ya 439 ya Sheria za Tanzania pamoja na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84(2)ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati iliwaalika wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Napenda Kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote walio Shiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutambua mchango wa wadau wafuatao Chama cha Mwakili wa Tanganyika, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Jukwaa la Sera Tanzania, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania na Kamati ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali, Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Fedha na Mipango na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitambua mchango maalumu wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa sababu ni Kamati inayoundwa na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kifungu cha 9 na inahusika moja kwa moja katika uchambuzi, upitishaji na utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mujibu wa sheria, sera, taratibu na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na madhumuni ya muswada ni kuwa maelezo ya jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyosomwa leo hapa Bungeni pamoja na maelezo yaliyomo kwenye Muswada kuanzia ukurasa wa nne mpaka wa saba

na kwa faida ya muda naomba maelezo haya yote ya sehemu hii yaingie kwenye *Hansard*, pamoja na maelezo yangu kuanzia ukurasa wa tano mpaka ukurasa wa saba yote yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mshauri wa Sheria wa Bunge na wadau mbalimbali waliofika kwenye Kamati. Kamati ilipitia kwa kina maoni yaliyotolewa na wadau na hasa maoni mbalimbali yaliyotolewa kuhusiana na marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una jumla ya Ibara 15 na umegawanyika katika sehemu kuu tatu. Kamati kwa umakini mkubwa ilipitia Ibara zote 15. Katika Ibara zote zilizochambuliwa na Kamati, Kamati ilijiridhisha kwamba kuna Ibara katika Muswada huu ambazo hazina tatizo lolote la kimaudhui na zinazojikita zaidi katika muundo (*construction provisions*). Ibara hizo ni kama ifuatavyo; Ibara ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya tisa, ya kumi na moja, ya kumi na mbili, ya kumi na tatu pamoja na Ibara ya kumi na nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Ibara ya tisa, marekebisho yanayofanyika ni maboresho ya kiuandishi ya neno "*port folio*" kama linavyosomeka katika Kifungu cha 62(2)(a) cha Sheria ya Bajeti na kuliandika tena ili lisomeke "*portfolio*" ili kulipa maana na mantiki iliyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iligundua pia yapo makosa ya mpangilio wa Ibara za Muswada ambao unafanya Ibara zilizopo zisomeke kuwa ni 14 badala ya 15. Ibara ya 11 ya Muswada imesomeka mara mbili na Ibara inayosomeka 11 katika sehemu ya tatu ya Muswada inatakiwa kusomeka kama Ibara ya 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia iligundua kwamba Muswada umeonyesha sehemu za kwanza na ya tatu ya Muswada lakini haujataja ipi ni sehemu ya pili ya Muswada. Kwa kanuni bora za uandishi na muundo wa Muswada ni vema sehemu ya pili ya Muswada ikaonekana katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilijiridhisha kwamba marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali utekelezaji wa majukumu, Sura ya 268 kama yalivyotajwa katika malengo na madhumuni ya Muswada ni marekebisho mazuri na yanayoleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kimsingi yaliungwa mkono na wadau wote pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ambazo zilihitaji majadiliano ya kina kati ya Serikali na Kamati ni Ibara za nne, tano, sita, saba, nane, kumi na kumi na moja. Ibara zote hizi kwa pamoja zina lengo la kuboresha muda wa Serikali kutoa taarifa ya utekelezaji Bajeti Bungeni kutoka miezi mitatu mpaka miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 41(7) cha Sheria hiyo kinachohusiana na uhamisho wa fedha (*reallocation*) na uwasilishaji wa taarifa za uhamisho huo Bungeni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za uhamisho wa fedha Bungeni kwa Waziri mwenye dhamana kutoka Robo mwaka (*quarterly*) hadi nusu mwaka (*mid-year*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 55(2) cha

Sheria ya Bajeti kuhusu uwasilishaji wa taarifa ya robo mwaka Bungeni kuhusu miadi ya matumizi ya kila kasma (*Report on Expenditure Commitment*). Marekebisho yanayopendekezwa ni kuwasilisha taarifa hii ya miadi ya matumizi ya kila kasma kutoka robo mwaka na kwenda nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza waziri mwenye dhamana ya fedha awasilishe Bungeni taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (*Compliance Report*) miezi sita baada ya kupitishwa kwa bajeti ya Serikali na kila mwisho wa mwaka wa fedha na siyo kila baada ya robo mwaka kama ilivyo sasa kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya kiuandishi katika maelezo ya pembeni (*marginal notes*)kwa kufuta maneno "*quarterly statements*" na badala yake kuweka "*mid-year statements*."

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inapendekezwa kuwa kifungu kidogo cha (1) kifutwe na kuandikwe upya ili taarifa ya mapato na matumizi halisi ya serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma iwasilishwe Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya fedha miezi sita baada ya kupitishwa kwa bajeti ya Serikali badala ya kila robo mwaka kama ilivyo katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 61 cha Sheria ya Bajeti ili kuweka masharti kuwa taarifa ya misamaha ya kodi iwasilishwe Bungeni kila nusu mwaka badala ya muda wa robo mwaka unaotajwa katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 63(2)(b)

kinachohusu uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Bungeni kila baada ya baada ya robo mwaka, kwa neno *"quarterly"* na kuweka badala yake neno *"mid-year."* Lengo la mapendekezo haya ni kuweka masharti yatakayowezesha taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kila baada ya nusu mwaka kama ilivyopendekezwa katika Ibara ya 6 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza kuwa Afisa wa Umma aliyesababishia Serikali au taasisi ya umma kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa makusudi au kwa uzembe chini ya Sheria ya Bajeti kifungu cha 65(2) awajibishwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na akatwe mshahara wa miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa maafisa husika wanatekeleza ipasavyo masharti ya Sheria ya Bajeti tofauti na Sheria ilivyo sasa ambapo afisa wa umma aliyetenda kosa hilo anachukuliwa hatua za kinidhamu tu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma bila kukatwa mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango yaliyotolewa kwenye Kamati, maboresho haya yanakusudia kutoa muda zaidi kwa Serikali kukusanya taarifa muhimu za utekelezaji wa bajeti kutoka kwa Serikali za Mitaa, Idara mbalimbali za Serikali na wahisani wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliarifiwa kwamba ili kuandaa ipasavyo taarifa za utekelezaji wa bajeti, Wizara na taasisi mbalimbali zinahitaji muda wa kutosha wa kukusanya takwimu, kuzifanyia uchambuzi na hatimaye kuandaa taarifa husika na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na

Mipango kwa uchambuzi na kuzijumuisha pamoja (*consolidation*) na kwamba muda wa robo mwaka uliopo hivi sasa kisheria hautoi fursa kwa taasisi na Wizara kukusanya takwimu sahihi na kuzifanyia uchambuzi ili kuandaa taarifa zenye kubainisha hali halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatia kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu marekebisho ya Sheria ya Bajeti, 2015, Sura ya 439 ambapo kutokana na majadiliano na muafaka uliofikiwa kati ya Serikali na Kamati, Kamati inashauri Serikali kuzingatia mambo yafuatayo katika marekebisho yanayokusudiwa:-

(i) Kwamba marekebisho haya yaongeze uwezo na fursa kwa Bunge kusimamia kwa wakati uhamishaji wa fedha (*reallocation of funds*) unaofanywa na Serikali na kuongeza uwajibikaji wa Serikali na uwezo wa Bunge kusimamia kwa karibu matumizi ya Serikali kwa kuzingatia vipaumbele, sheria, uwepo na tija ya matumizi husika.

(ii) Marekebisho haya yaongeze uwezo wa Bunge kugundua kwa haraka vipaumbele ambavyo havijatekelezwa, matumizi yasiyo na tija, vyanzo vya mapato visivyofanya vizuri na upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

(iii) Marekebisho yanayokusudiwa yatoe nafasi/fursa kwa Bunge kujadili na kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kutekeleza bajeti kwa kuzingatia changamoto zilizoonekana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa miaka ya fedha iliyotangulia.

(iv) Marekebisho haya yatoe nafasi kwa Bunge kupata kwa wakati taarifa ya misamaha ya kodi, tozo na ada nyingineze.

(v) Katika Ibara ya 11 ya Muswada ambayo inabadilisha Kifungu 65(2) cha Sheria ya Bajeti, Kamati inashauri kwamba adhabu inayopendekezwa kwa Afisa wa Umma aliyetenda makosa yaliyotajwa chini ya kifungu hiki ama kwa uzembe au kwa kukusudia iongezwe; kwanza, kukata mshahara wa mtumishi huyo wa umma kwa miezi sita na pili, iwe ni kwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyingine za jinai za nchi. Kamati inashauri kifungu hiki Kisomeke ifuatavyo:-

“Subject to a deduction of six months’ salary and other disciplinary measures in accordance with the Public Service Act and other relevant criminal laws of the land.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itaongeza mawanda ya adhabu kwa watumishi wa umma wanaokwamisha utekelezaji wa bajeti kwa makusudi au kwa uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nafasi maalum ya kamati ya Bunge ya bajeti katika kusimamia utekelezaji wa bajeti ya serikali. Ninaomba iingie katika rekodi rasmi ya Bunge hili kwamba marekebisho haya hayataondoa nafasi na mamlaka ya Kikatiba na Kisheria ya Kamati ya Bajeti ya Bunge katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (*oversight function of the National Assembly*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha tisa cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Bajeti inaweza kupata taarifa za awali za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha miezi mitatu baada ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuanza katika kila mwaka mpya wa fedha kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(j)(h) cha Sheria ya Bajeti kinatamka ifuatavyo:-

"The Parliamentary Budget Committee shall, in addition to functions provided under the Parliamentary Standing Orders, carry out the following functions..."

"(h) in relation to oversight responsibility, discharge or perform any function as spelt out under the Parliamentary Standing Orders."

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinatoa mamlaka kwa Kamati ya bajeti kuendelea kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Kwa msingi huu, pamoja na marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa Kamati ya Bajeti ya Bunge kila inapohitajika kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 9(d) ya Sehemu ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati inakubaliana na marekebisho yote yaliyomo katika Muswada huu kuhusu Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na inaamini kwamba marekebisho hayo yataleta tija katika kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, pia naomba Bunge lako litambue kwamba kamati mpaka hivi sasa imekwishasoma taarifa tisa ambayo ni rekodi kubwa kabisa kutokea kati ya Kamati zote za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Pia niwashukuru Wajumbe waalikwa wa Kamati ya Bajeti ya Bunge kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majina ya wajumbe walioshiriki kwenye uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuu watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kasilillah kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* Ndugu Hanifa Masaninga, Makatibu wote Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Stella Bwimbo, Ndugu Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rachel Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI, (NA. 1) WA MWAKA
2017, THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)
BILL, NO. 1 OF 2017 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI:

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 wa Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.1) Act of 2017.

1.2 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni kikao cha mwisho cha Mkutano huu wa saba wa Bunge la 11, kabla sijaingia katika masuala ya msingi ya Muswada huu, napenda kukupongeza kwa dhati wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia kwa umahiri Shughuli zote za Bunge hili la Kumi na Moja. Bunge hili sasa limeingia katika Historia hasa kwa kupitisha Miswada Miwili ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill*) na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*) pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2017.

1.3 Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zote zinawakilisha Tanzania mpya. Hongera sana Mheshimiwa Spika kwa kufanikisha suala hili kupitia Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu mwezi Janauri, 2017 baada

ya kusomwa bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Sita wa Bunge ili iufanyie kazi, na mnamo tarehe 07 Machi, 2017, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango walifika mbele ya Kamati iliyoketi Dodoma na kutoa maelezo kuhusu malengo na Madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho mbalimbali ya msingi katika Sheria husika kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Fedha na Mipango kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo ya kina kuhusu sababu za serikali kupendekeza marekebisho haya ya Sheria, majadiliano ya kina kati ya Serikali, kamati za Bunge na Taasisi nyingine yaliendelea kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, siku ya jana tarehe 04 Julai, 2017 Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango walifika kwa mara nyingine tena mbele ya Kamati ili kutoa majibu ya hoja za Kamati na wadau mbalimbali kutokana na vikao vya kujadili mapendekezo ya marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ni matokeo muafaka uliofikiwa kati ya Kamati na Serikali kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuanzia Mwaka huu wa fedha 2017/2018 ambao utaleta tija katika utekelezaji wa bajeti.

1.4 Mheshimiwa Spika, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni:

(i) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Sura ya 439 ya Sheria za Tanzania

(ii) Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania;

1.5 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

1.6 Napenda Kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliohiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu.

Naomba kutambua mchango wa wadau wafuatao:-

- i) Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS),
- ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),
- iii) Jukwaa la Sera Tanzania (Policy Forum-PF),
- iv) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF),
- v) Kamati ya Bunge ya Bajeti (PBC),

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Serikali Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Fedha na Mipango na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitambua mchango maalumu wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa sababu ni Kamati inayoundwa na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Kifungu cha 9 na inahusika moja kwa moja katika uchambuzi, upitishaji na utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Sheria, Sera, Taratibu na Kanuni zilizopo.

2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyosomwa leo hapa Bungeni pamoja na maelezo yaliyomo kwenye Muswada kuanzia Ukurasa wa Nne mpaka wa Saba na kwa faida ya muda naomba maelezo haya yote ya sehemu hii yaingie kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268. Marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika Katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Muswada, na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa Kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza kuifanyia Marekebisho Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Marekebisho yanapendekeza kufanyia marekebisho katika Vifungu vya 41 (7), 53(2), 56(1), (7), 57, 61, 62 na 63 kwa lengo la kuiwezesha Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa za uhamisho wa fedha, taarifa za matumizi, taarifa za utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha mbalimbali ya kodi na taarifa za mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ilivyoainishwa kwenye vifungu tajwa.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho haya yanalenga kuipatia Serikali muda wa kutosha kukusanya na kupitia taarifa hizo kabla ya kuziwasilisha Bungeni. Aidha, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 65(2) kwa lengo la kuongeza adhabu kwa maafisa wa umma watakaokiuka masharti ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268. Marekebisho hayo yanapendekezwa katika vifungu vya 8, kichwa cha Sehemu ya Saba na kifungu cha 17(1) ambayo yanaondoa mapungufu ya kiuandishi. Dhamira ni kwenda sambamba na marekebisho yaliyofanywa mwaka 2002 na 2009. Marekebisho hayo yaliondoa neno "Ordinance" na

kuweka neno "Act". Aidha, yalifuta Sheria ya Uasili na badala yake kutunga Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Vile vile, inapendekezwa kufanya marekebisho ya kiuhariri katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 17.

3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Sheria wa Bunge na Wadau mbalimbali waliofika kwenye Kamati. Kamati ilipitia kwa kina maoni yaliyotolewa na wadau na hasa maoni mbalimbali yaliyotolewa kuhusiana na marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una jumla ya Ibara 15 na umegawanyika katika Sehemu Kuu tatu. Kamati kwa umakini mkubwa ilipitia Ibara zote 15. Katika Ibara zote zilizochambuliwa na Kamati, Kamati ilijiridhisha kwamba kuna Ibara katika Muswada huu ambazo hazina tatizo lolote la kimaudhui na zinazojikita zaidi katika Muundo. (Construction Provisions). Ibara hizo ni kama lfuatavyo; Ibara ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya tisa, ya kumi na moja, ya kumi na mbili, ya kumi na tatu pamoja na Kumi na Nne.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Ibara ya Tisa, Marekebisho yanayofanyika ni maboresho ya kiuandishi ya neno "*port folio*" kama linavyosomeka katika Kifungu cha 62(2)(a) cha Sheria ya Bajeti na kuliandika tena ili lisomeke "*portfolio*" ili kulipa maana na mantiki iliyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iligundua pia yapo makosa ya mpangilio wa Ibara za Muswada ambao unafanya Ibara zilizopo zisomeke kuwa ni 14 badala ya 15. Ibara ya 11 ya Muswada imesomeka mara mbili na Ibara inayosomeka 11 katika sehemu ya Tatu ya Muswada inatakiwa kusomeka kama Ibara ya 12. Kamati pia iligundua

kwamba Muswada umeonyesha Sehemu za Kwanza na za Tatu za Muswada lakini haujataja ipi ni sehemu ya pili ya Muswada. Kwa Kanuni Bora za Uandishi na Muundo wa Muswada ni vema Sehemu ya Pili ya Muswada ikaonekana katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilijiridhisha kwamba marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268 kama yalivyotajwa katika Malengo na Madhumuni ya Muswada ni marekebisho mazuri na yanayoleta tija katika utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho yanayokusudiwa kufanywa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kimsingi yaliungwa mkono na wadau wote pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ambazo zilihitaji majadiliano ya Kina kati ya Serikali na Kamati ni Ibara ya Nne, Tano, Sita, Saba, Nane, Kumi na Kumi na Moja. Ibara zote hizi kwa pamoja zina lengo la kuboresha muda wa Serikali kutoa taarifa ya utekelezaji Bajeti Bungeni kutoka Miezi 3 mpaka miezi 6.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 41(7) cha Sheria hiyo kinachohusiana na uhamisho wa fedha (Reallocation) na uwasilishaji wa taarifa za uhamisho huo Bungeni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za Uhamisho wa fedha Bungeni kwa Waziri mwenye dhamana kutoka Robo mwaka (Quartely) hadi Nusu mwaka (Mid-Year).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 53(2) cha Sheria ya Bajeti kuhusu uwasilishaji wa Taarifa ya Robo Mwaka

Bungeni kuhusu Miadi ya Matumizi ya Kila Kasma (Report on Expenditure Commitment). Marekebisho yanayopendekezwa ni kuwasilisha taarifa hii ya miadi ya matumizi ya kila Kasma kutoka Robo mwaka na kwenda Nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza waziri mwenye dhamana ya Fedha awasilishe Bungeni taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (Compliance Report) miezi sita baada ya kupitishwa kwa bajeti ya Serikali na kila mwisho wa mwaka wa fedha na siyo kila baada ya Robo mwaka kama ilivyo sasa kwenye Sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza kufanya Marekebisho ya kiuandishi katika maelezo ya Pembeni (Marginal Notes) kwa kufuta maneno "Quarterly Statements" na badala yake kuweka "Mid-Year Statements". Pia inapendekezwa kuwa kifungu kidogo cha (1) kifutwe na kuandikwa upya ili taarifa ya mapato na matumizi halisi ya serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma iwasilishwe Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya fedha miezi sita baada ya kupitishwa kwa bajeti ya Serikali badala ya kila robo mwaka kama ilivyo katika Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 61 cha Sheria ya Bajeti ili kuweka masharti kuwa taarifa ya misamaha ya Kodi iwasilishwe Bungeni kila nusu mwaka badala ya muda wa robo mwaka unaotajwa katika Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 63(2) (b) kinachohusu uwasilishaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Bungeni kila baada ya baada ya Robo Mwaka, kwa neno "Quarterly" na kuweka badala yake neno "Mid-year". Lengo la Mapendekezo haya ni kuweka masharti

yatakayowezesha taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kila baada ya nusu mwaka kama ilivyopendekezwa katika Ibara ya 6 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza kuwa afisa wa umma aliyesababishia Serikali au Taasisi ya Umma kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa makusudi au kwa uzembe chini ya Sheria ya Bajeti Kifungu cha 65(2) awajibishwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na akatwe mshahara wa miezi sita. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa maafisa husika wanatekeleza ipasavyo Masharti ya Sheria ya Bajeti tofauti na Sheria ilivyo sasa ambapo afisa wa umma aliyetenda kosa hilo anachukuliwa hatua za kinidhamu tu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma bila kukatwa Mshahara wake.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango yaliyotolewa kwenye Kamati, maboresho haya yanakusudia kutoa muda zaidi kwa serikali kukusanya taarifa muhimu za utekelezaji wa bajeti kutoka wa serikali za mitaa, idara mbalimbali za serikali na wahisani wa maendeleo. Kamati iliirifiwa kwamba ili kuandaa ipasavyo taarifa za utekelezaji wa bajeti, Wizara na Taasisi mbalimbali zinahitaji muda wa kutosha wa kukusanya takwimu, kuzifanyia uchambuzi na hatimaye kuandaa taarifa husika na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi na kuzijumuisha pamoja (Consolidation) na kwamba muda wa Robo mwaka uliopo hivi sasa kisheria hautoi fursa kwa taasisi na wizara kukusanya takwimu sahihi na kuzifanyia uchambuzi ili kuandaa taarifa zenye kubainisha hali halisi ya utekelezaji wa bajeti ya serikali.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

KUHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA YA BAJETI, 2015, SURA YA 439

4.1 Mheshimiwa Spika, kutokana na majadiliano na muafaka uliofikiwa kati ya Serikali na Kamati, Kamati inashauri Serikali kuzingatia mambo yafuatayo katika marekebisho yanayokusudiwa;

i) Kwamba marekebisho haya yaongeze uwezo na fursa kwa Bunge kusimamia kwa wakati uhamishaji wa fedha (Reallocation of funds) unaofanywa na Serikali na kuongeza uwajibikaji wa Serikali na uwezo wa Bunge kusimamia kwa karibu matumizi ya Serikali kwa Kuzingatia vipaumbele, Sheria, uwepo na tija ya matumizi husika.

ii) Marekebisho haya yaongeze uwezo wa Bunge kugundua kwa haraka vipaumbele ambavyo havijatekelezwa, matumizi yasiyo na tija, vyanzo vya mapato visivyofanya vizuri na upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

iii) Marekebisho yanayokusudiwa yatoe nafasi/fursa kwa Bunge kujadili na kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kutekeleza Bajeti kwa kuzingatia changamoto zilizoonekana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali miaka ya fedha iliyotangulia.

iv) Marekebisho haya yatoe nafasi kwa Bunge kupata kwa wakati Taarifa ya misamaha ya kodi, tozo na ada nyingineze.

v) Katika Ibara ya 11 ya Muswada ambayo inabadilisha Kifungu 65(2) cha Sheria ya Bajeti, Kamati inashauri kwamba adhabu inayopendekezwa kwa afisa wa umma aliyetenda makosa yaliyotajwa chini ya Kifungu hiki ama kwa uzembe au kwa kukusudia iongezwe kwa ; kwanza kukata mshahara wa mtumishi huyo wa umma kwa miezi Sita na; pili iwe ni kwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria nyingine za Jinai za nchi. Kamati inashauri Kifungu hiki Kisomeke ifuatavyo;

'Subject to a deduction of six months' salary and other disciplinary measures in accordance with the Public Service Act and other relevant criminal laws of the land.' Hatua hii itaongeza mawanda ya adhabu kwa watumishi wa umma wanaokwamisha utekelezaji wa bajeti kwa makusudi au kwa uzembe

4.2 NAFASI MAALUMU YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KATIKA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, ninaomba iingie katika rekodi rasmi ya Bunge hili kwamba marekebisho haya hayataondoa nafasi na mamlaka ya Kikatiba na Kisheria ya Kamati ya Bajeti ya Bunge katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (Oversight Function of the National Assembly). Kwa mujibu wa Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Bajeti *inaweza kupata taarifa za awali* za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha miezi mitatu baada ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuanza katika kila mwaka mpya wa Fedha kuanza.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha **9 (j)(h)** cha Sheria ya Bajeti kinatamka ifuatavyo; *'The Parliamentary Budget Committee Shall, in addition to functions provided under the Parliamentary Standing Orders, carry out the following functions.....(h) in relation to oversight responsibility, discharge or perform any function as spelt out under the Parliamentary Standing Orders'*

Mheshimiwa Spika, Kifungu hiki kinatoa mamlaka kwa Kamati ya bajeti kuendelea kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Kwa msingi huu, pamoja na marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa Kamati ya Bajeti ya Bunge

kila inapohitajika kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya **9(d)** ya Sehemu ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

4.3 KUHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTEKELEZAJI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

vi) Kamati inakubaliana na marekebisho yote yaliyomo katika Muswada huu kuhusu Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali na inaamini kwamba marekebisho hayo yataleta tija katika kutekeleza majukumu ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa wa Kamati ya Bajeti ya Bunge kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha.

Naomba Majina ya wajumbe walioshiriki kwenye uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe

6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Ussi Pondeza, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Wanou Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Taska Mbogo, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashiillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

JULAI 5 2017

NAIBU SPIKA: Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Katiba na Sheria.

MHE. HAMIDU H. BOBALI- (K.n.y. MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Marekebisho wa Sheria Mbalimbali Namba 1 wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 1 juzuu ya 98 tarehe 12 Januari, 2017. Kwa ujumla wake Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura 439 na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura 268.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura 439 ya mwaka 2015. Muswada wa Sheria ya Bajeti ulichapishwa tarehe 31 Oktoba, 2014 kwenye Gazeti la Serikali namba 13 ambapo ulikuwa umesainiwa na Waziri wa Fedha wa wakati huo Mheshimiwa Saada M. Salum tarehe 27 Oktoba, 2014. Ni wazi kuwa kati ya mafanikio makubwa ya Bunge la Kumi ni pamoja na kutungwa na hatimaye kuanza kutekelezwa kwa sheria hii ambayo ni msingi mkubwa wa utekelezaji wa majukumu ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 ilipitishwa na Bunge na baadae kuridhiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na kwa ajili ya utekelezaji na kuwa Sura 439.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu sehemu ya madhumuni na sababu zilizopelekea kutungwa sheria hiyo kama ifuatavyo:-

"This Bill proposes for the enactment of the Budget Act with a view to put in place legal framework for management of the Government budget process from preparation, approval, execution, monitoring, evaluation and reporting.

The Bill intends to put in place a better system between the Government, National Assembly and other entities involved in the budget process, existence of budget discipline by observing plans, revenue and expenditure, a credible budget which is implemented as approved by the National Assembly and putting in place special arrangement for handling reallocation of funds. In addition, the Bill expects to incorporate the budgets of Public entities in the books for the Estimates of Public Revenue and Expenditure respectively."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari na tafsiri isiyo rasmi madhumuni na sababu za kutungwa kwa sheria hii zilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka utaratibu wa kisheria kwa ajili ya kusimamia mchakato wa Bajeti ya Serikali kuanzia wakati wa maandalizi, kuidhinishwa, utekelezaji, usimamizi, tathmina na utoaji wa taarifa za kibajeti.

(ii) Kuweka mfumo bora wa kibajeti kati ya Bunge na Serikali.

(iii) Kuzingatia misingi na mipango ya kibajeti kama ilivyopitishwa na Bunge.

(iv) Kuweka utaratibu wa kuhamisha mafungu ya Bajeti ya Serikali (*reallocation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2) inasema kama ifuatavyo na naomba kunukuu:-

"Sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na

madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimerejea madhumuni na sababu zilizopelekea kutungwa kwa Sheria ya Bajeti pamoja na majukumu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba kwa sababu Muswada ulioko mbele yako leo unapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali kuhusu masuala ya matumizi ya fedha za Serikali zinazopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma madhumuni na sababu za kuletwa kwa Muswada huu hasa Sehemu ya Pili ya Muswada ambayo inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bajeti Sura ya 439 katika vifungu vya 47(7), 53(2), 56(1) na 7, 57, 61, 62 na 63 na Serikali imeleta marekebisho haya kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa ya uhamisho wa fedha, taarifa ya matumizi, taarifa ya utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha ya kodi na taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ulivyo utaratibu wa kisheria wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka wazi kuwa haiungi mkono marekebisho yote kwenye Sheria ya Bajeti kwa sababu marekebisho haya ya Sheria ya Bajeti yatapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali. Hii ni kutokana na matendo ya Serikali hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka wazi kuwa, haiungi mkono marekebisho yote kwenye Sheria ya Bajeti kwa sababu marekebisho haya ya Sheria ya Bajeti yatapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali. Hii ni kutokana na matendo ya Serikali hii kama ifuatavyo:-

(i) Bunge linakaa Mikutano minne kwa mwaka na au vikao vya dharura ambavyo vinaweza kuitishwa kwa mujibu wa Katiba. Kuweka masharti ya taarifa za matumizi ya fedha na masharti yote ya kibajeti kuwasilishwa kila baada ya miezi sita ni kuipoka Kamati ya Bajeti mamlaka yake na Bunge kwa ujumla kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya kibajeti. Bunge lisipokuwa makini itakuja hoja ya kubadili Katiba ya nchi na kupunguza Mikutano ya Bunge kwa mwaka ili kuipa Serikali muda wa kutekeleza Bajeti. *(Makofi)*

(ii) Hata katika Halmashauri Kamati za Fedha na Uchumi hukaa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kusimamia Halmashauri zetu, ni kwa nini Serikali hii ambayo imepoka vyanzo muhimu vya mapato vya Halmashauri zetu kwenda Serikali kuu isisimamiwe na Bunge kila baada ya miezi sita? *(Makofi)*

(iii) Serikali hii ambayo takwimu za vitabu vya mapato na matumizi zinatofautiana kwa miaka miwili mfululizo na Serikali iko kimya hata baada ya kuelezwa hivyo na Kambi Rasmi ya Upinzani, je itaaminika vipi kupewa miezi sita kwa ajili ya kuleta taarifa mbalimbali za kibajeti ndani ya Bunge? *(Makofi)*

(iv) Ni Serikali ipi inayotaka kupewa muda wa miezi sita ya kuwasilisha taarifa za fedha na masharti mengine ya Kibajeti au ni Serikali hii ya CCM ambayo kumekuwa na tabia ya kuahidi kwenye mikutano ya hadhara kutoa mabilioni ya fedha bila kuzingatia Bajeti ambayo imepitishwa na Bunge? *(Makofi)*

(v) Je, ni Serikali hii ambayo imepunguza Bajeti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na hivyo kumfanya ashindwe kwa ukamilifu wake ndiyo inayotaka iongezewe muda wa kuwasilisha taarifa za kibajeti Bungeni? *(Makofi)*

(vi) Ni Serikali ipi inayotaka kuongezewa muda wa kuwasilisha taarifa za kibajeti kwenye Bunge au ni Serikali hii

ambayo inatoa fedha za kununulia ndege kwa ajili ya malipo ya awali na fedha hizo hazijulikani zilitoka kwa utaratibu gani wa kibajeti? *(Makofi)*

(vii) Ni Serikali gani ambayo bila aibu inatoa kauli kuwa Rais ndiye mwenye fedha za Serikali na huku ikijulikana kuwa Serikali hupata fedha zake zote kutokana na kukusanya kodi kutoka kwa wananchi pamoja na mikopo na misaada ya kibajeti kutoka nchi wahisani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati huu ambao Bunge linatakiwa kuonesha wivu wa madaraka yake kwa vitendo. Kwa jinsi ilivyo sasa na mapendekezo haya ya Muswada ulivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa kupitishwa kwa Muswada huu utakuwa ni mwanzo wa kuanza kushuka kwa dhana na uwajibikaji wa Serikali kwa muhimili huu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 65(2) ambacho kinatoa adhabu kwa mtumishi wa umma ambaye atakiuka masharti ya Sheria ya Bajeti kwa kuongeza adhabu ya kukatwa mshahara wa miezi sita pamoja na hatua zingine za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kifungu hicho kibaki kama ilivyokuwa awali kwa sababu kusema kuwa yafanyike makato ya mshahara wa mtumishi kwa miezi sita bila kuzingatia hasara ambayo anaweza kuisababisha haitakuwa na maana yoyote. Kambi Rasmi inapendekeza hatua za nidhamu kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi wa umma na kama kuna makosa ya jinai hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali, Utekelezaji wa Majukumu, Sura ya 268 ili kuondoa mapungufu ya kiuandishi, kiuhariri na pia kuzingatia kutungwa kwa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na marekebisho haya, lakini Serikali makini ilitakiwa kufanya wakati wa kutunga Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kwa sababu Sheria mpya inapotungwa, inatungwa kwa kuzingatia sheria zingine zote za nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Sheria mpya zinapoletwa Bungeni zifanyiwe uchambuzi ili kuhakikisha kuwa zinaendana na sheria zingine zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU (MB) KUHUSU MUSWADA WA
MAREKEBISHO WA SHERIA MBALIMBALI NAMBA 1 WA
MWAKA 2017 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**“Inatolewa Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu
za Bunge, Toleo la Januari, 2016”**

1. Utangulizi _____

Mheshimiwa Spika, Muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 1 juzuu ya 98 tarehe 12 Januari, 2017. Kwa ujumla wake muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura 439 na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura 268.

2. Marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura 439 ya Mwaka 2015

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Bajeti ulichapishwa 31 Oktoba, 2014 kwenye Gazeti la Serikali namba 13 ambapo ulikuwa umesainiwa na Waziri wa Fedha wa wakati huo Mheshimiwa Saada M. Salum tarehe 27 Oktoba mwaka 2014. Ni wazi kuwa kati ya mafanikio makubwa ya Bunge la kumi ni pamoja na kutungwa na hatimaye kuanza kutekelezwa kwa sheria hii ambayo ni msingi mkubwa wa utekelezaji wa majukumu ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, Baadae Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 ilipitishwa na Bunge na baadae kuridhiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na kwa ajili ya utekelezaji na kuwa sura 439.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya madhumuni na sababu zilizopelekea kutungwa sheria hiyo kama ifuatavyo;

“This Bill proposes for the enactment of the Budget Act with a view to put in place legal framework for management of the Government budget process from preparation, approval, execution, monitoring, evaluation and reporting.

The Bill intends to put in place a better system between the Government, National Assembly and other entities involved in the budget process, existence of budget discipline by observing plans, revenue and expenditure, a credible budget which is implemented as approved by the National Assembly and putting in place special arrangement for handling reallocation of funds. In addition, the Bill expects to incorporate the budgets of Public entities in the books for the Estimates of Public Revenue and Expenditure respectively.”

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari na tafsiri isiyo rasmi madhumuni na sababu za kutungwa kwa Sheria hii zilikuwa kama ifuatavyo;

(i) Kuweka utaratibu wa kisheria kwa ajili ya kusimamia mchakato wa Bajeti ya Serikali kuanzia wakati wa maandalizi, kuidhinishwa, utekelezaji, usimamizi, tathimina na utoaji wa taarifa za kibajeti.

(ii) Kuweka mfumo bora wa kibajeti kati ya Bunge na Serikali

(iii) Kuzingatia misingi na mipango ya kibajeti kama ilivyopitishwa na Bunge

(iv) Kuweka utaratibu wa kuhamisha mafungu ya Bajeti ya Serikali (reallocation).

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 63(2) inasema kama ifuatavyo; naomba kunukuu,

“Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.”

Mheshimiwa Spika, nimerejea madhumuni na sababu zilizopelekea kutungwa kwa Sheria ya Bajeti pamoja na majukumu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba kwa sababu Muswada ulioko mbele yako leo unapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali kuhusu masuala ya matumizi ya fedha za Serikali zinazopitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma madhumuni na sababu za kuletwa kwa muswada huu hasa sehemu ya pili ya Muswada ambao inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 katika vifungu vya 47(7), 53(2), 56(1) na 7, 57, 61, 62 na 63 na Serikali imeleta marekebisho hayo kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa ya uhamisho wa fedha, taarifa ya matumizi, taarifa ya utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha ya kodi na taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ulivyo utaratibu wa kisheria wa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka wazi kuwa haiungi mkono marekebisho yote kwenye Sheria ya Bajeti kwa sababu marekebisho haya ya Sheria ya Bajeti yatapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali. Hii ni kutokana na matendo ya Serikali hii kama ifuatavyo;

(i) Bunge linakaa Mikutano minne kila mwaka na au vikao vya dharura ambavyo vinaweza kuitishwa kwa mujibu wa Katiba. Kuweka masharti ya taarifa za matumizi ya fedha na masharti yote ya Kibajeti kuwasilishwa kila baada ya miezi sita ni kuipoka Kamati ya Bajeti mamlaka yake na Bunge kwa ujumla kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya kibajeti. Bunge lisipokuwa makini itakuja hoja ya kubadili Katiba ya nchi na kupunguza mikutano ya Bunge kwa mwaka ili kuipa Serikali muda wa kutekeleza Bajeti.

(ii) Hata katika Halmashauri Kamati za Fedha na Uchumi hukaa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kusimamia Halmashauri zetu, ni kwa nini Serikali hii ambayo imepoka vyanzo muhimu vya mapato vya Halmashauri zetu kwenda Serikali kuu isisimamiwe na Bunge kila baada ya miezi mitatu?

(iii) Serikali hii ambayo takwimu za vitabu vya mapato na matumizi zinatofautiana kwa miaka miwili mfululizo na

Serikali iko kimya hata baada ya kuelezwa hivyo na Kambi Rasmi ya Upinzani, je itaaminika vipi kupewa miezi sita kwa ajili ya kuleta taarifa mbalimbali za kibajeti ndani ya Bunge?

(iv) Ni Serikali ipi inayotaka kupewa muda wa miezi sita ya kuwasilisha taarifa za fedha na masharti mengine ya Kibajeti au ni Serikali hii ya CCM ambayo kumekuwa na tabia ya kuahidi kwenye mikutano ya hadhara kutoa mabilioni ya fedha bila kuzingatia Bajeti ambayo imepitishwa na Bunge.

(v) Je, ni Serikali hii ambayo imepunguza Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na hivyo kumfanya ashindwe kwa ukamilifu wake ndiyo inayotaka iongezewe muda wa kuwasilisha taarifa za kibajeti Bungeni?

(vi) Ni Serikali ipi inayotaka kuongezewa muda wa kuwasilisha taarifa za kibajeti kwenye Bunge, au ni Serikali hii ambayo inatoa fedha za kununulia Ndege kwa ajili ya malipo ya awali na fedha hizo hazijulikani zilitoka kwa utaratibu gani wa kibajeti?

(vii) Ni Serikali gani ambayo bila aibu inatoa kauli kuwa Rais ndiye mwenye fedha za Serikali na huku ikijulikana kuwa Serikali hupata fedha zake zote kutokana na kukusanya kodi kutoka kwa wananchi pamoja na mikopo na misaada ya kibajeti kutoka nchi wahisani?

Mheshimiwa Spika, ni wakati huu ambao Bunge linatakiwa kuonesha wivu wa madaraka yake kwa vitendo, kwa jinsi ilivyo sasa na mapendekezo haya ya Muswada ulivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa kupitishwa kwa muswada huu utakuwa ni mwanzo wa kuanza kushuka kwa dhana na uwajibikaji wa Serikali kwa muhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 65(2) ambacho kinatoa adhabu kwa mtumishi wa umma ambaye atakiuka masharti

ya Sheria ya Bajeti kwa kuongeza adhabu ya kukatwa mshahara wa miezi sita pamoja na hatua zingine za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kifungu hicho kibaki kama ilivyokuwa awali kwa sababu kusema kuwa yafanyike makato ya mshahara wa mtumishi kwa muda wa miezi sita bila kuzingatia hasara ambayo anaweza kuisababisha haitakuwa na maana yoyote. Kambi Rasmi inapendekeza hatua za nidhamu kwa mujibu wa Sheria na taratibu za Utumishi wa umma na kama kuna makosa ya jinai hatua zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria hizo.

3. Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura ya 268

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura ya 268 ili kuondoa mapungufu ya kiuandishi, kiuhariri na pia kuzingatia kutungwa kwa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na marekebisho haya lakini Serikali makini ilitakiwa kuyafanya wakati wa kutunga sheria ya Mtoto mwaka 2009 kwa sababu Sheria mpya inapotungwa, inatungwa kwa kuzingatia Sheria zingine zote za nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Sheria mpya zinapoletwa Bungeni zifanyiwe uchambuzi ili kuhakikisha kuwa zinaendana na Sheria zingine zilizopo.

HAMIDU HASSAN BOBALI (MB)
K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
WIZARA YA SHERIA NA KATIBA
05.07.2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji, tumemaliza mawasilisho baada ya kumsikiliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, sasa ninayo matangazo ambayo asubuhi yalikuwa hayajatangazwa.

Mheshimiwa Rehani, tafuta kiti ukae, mimi nimesimama hapa na wewe nakuona unazunguka.

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Shaabani Shekilindi ambao tangazo lao lilikuwa halijafika, na hawa wanatoka Lushoto ni wanamazingira wanatoka *Friends of Usambara*, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao wameongozwa na Ndugu Zuberi Mewile, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine ni habari ambazo pengine mlizisikia! Mnatangiwa kuwa Dkt. Tonia Kandiero, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*Africa Development Bank*), Kanda ya Afrika Kusini, alifariki tarehe 28 Juni, 2017 huko Pretoria yaani Tshwane, Afrika ya Kusini.

Kabla ya uteuzi huo aliwahi kuwa Mwakilishi Mkaazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*Africa Development Bank*) kuanzia mwaka 2011 hadi Novemba, 2016. Katika kipindi hicho alitoa mchango mkubwa sana wa kuwezesha upatikanaji wa fedha kupitia *African Development Bank* kwa ajili ya miradi ya maendeleo nchini, hususan miradi ya barabara na umeme; kwa mfano barabara ya Dar es Salaam – Iringa, barabara ya Dodoma – Babati, barabara ya Namtumbo – Tunduru – Mtambaswala na barabara ya Arusha – Taveta – Voi.

Kutokana na mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kwenda kusaini kitabu cha maombolezo

kilichopo Wizara y Fedha na Mipango - Hazina, hapa Dodoma kwa ajili ya kutoa salamu za rambirambi kwa msiba huo ambao umetupata. Tangazo limeletwa na Ofisi ya Utawala ya Bunge.

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji na nimeletewa majina hapa kutika vyama, kama tulivyo humu Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Mwita Waitara ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu sana kwa maslahi ya Watanzania. Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukiuangalia ni Muswada ambao unatoa fursa pana kwa Serikali kuongeza ufanisi katika utendaji wake. Katika mfumo wa kawaida wa kiutendaji kwa Waheshimiwa Wabunge ambao mna uzoefu kidogo wa kufanya kazi na taasisi kubwa utagundua kwamba, kunakuwa na taarifa za aina mbili; kuna taarifa za menejimenti, lakini kuna taarifa za *governance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *level* ya menejimenti ni taarifa ambazo zinatolewa katika ngazi ya taasisi husika katika muda wa miezi mitatu, ili kuiruhusu menejimenti iweze kujitathmini na iweze kuji-*re-orient* kufuatana na mahitaji na hali halisi ya wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapokuja kwenye *level* ya *governance* taarifa ile inatakiwa kwa kweli iwe imeshiba kidogo na iwe imejitosheleza kwa maana ya kwamba hata menejimenti yenyewe imepata nafasi ya kujitathmini na kuji-*orient* ili kuendena na malengo yaliyokusudiwa.

Sasa sisi Waheshimiwa Wabunge ni *level* ya juu sana ya utendaji wa Taifa hili. Katika mfumo nilioueleza sisi Wabunge tungejiweka katika *level* ya *governance*. Sasa tunapotaka kupata ripoti kila miezi mitatu ni kama vile ambavyo tunajiweka kwenye *level* ya menejimenti *on daily basis*. Kwa hiyo, mimi nikubaliane kabisa na Serikali kwamba kwa Muswada huu sasa haya mapendekezo yanayoletwa kwenye hizi sheria yakubaliwe na Wabunge na yaweze kuboresha utendaji wa Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sura ya 439, Ibara ya 4 mpaka ya 11 nimeshangazwa kidogo na Hotuba ya Kambi ya Upinzani inayotutaka sisi Wabunge au sisi kama Taifa tuwe sawa na mnyama anayeitwa nyumbu! Ukienda katika mbuga za wanyama kuna wanyama wawili, wale mtakaobahatika kwenda katika mbuga za wanyama kujifunza kidogo, kuna aina za wanyama wawili ambao wanaweza kukupa somo zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mnyama anaitwa nyumbu na kuna mnyama anaitwa nyati. Ukikutana na nyati anasafiri, anasafiri na kundi, katika kundi wanakwenda, wanasimama, wanaangalia mbele, wanaangalia nyuma, wanajipima, wanatafakari, wanasahihisha makosa, wanapiga hatua wanasonga mbele. Lakini ukimkuta mnyama nyumbu ameamua kwenda, basi atakwenda hata kama kuna makorongo, hata kama kuna nini, atatumbukia ataendelea na safari.

Sasa sisi Wabunge sio nyumbu, tumetekelza mfumo huu wa zamani wa *quarterly reports*, tumejifunza changamoto zinazotokana na mfumo huu, kwa sehemu kubwa Serikali imetumia muda mwingi kukaa kuandika ripoti kuliko kutekeleza majukumu waliyotumwa na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejifunza nini katika huo mfumo; ufanisi wetu ulikuwa mdogho sana. Leo tumekaa tumeona hilo tatizo tunaamua kuli-*focus*, tunapoli-*focus*

tunabadilisha huo mfumo tuiache Serikali ifanye kazi na menejimenti, wajipime wao ndani ya taasisi zao kwa miezi mitatu, halafu waende tena miezi mitatu, baada ya miezi mitatu mingine watuletee hapa ripoti iliyoshiba na inayojitoshesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangazwa kwa taarifa ya Upinzani wanasema mamlaka ya Bunge yamefunguzwa. Lazima tutofautishe kati ya mamlaka na ufanisi. Mamlaka yanakuwa na tija tu pale ambapo pana ufanisi mzuri wa kazi. Sasa kama mamlaka yako wewe kama Bunge yana-*compromise* ufanisi katika Serikali, mamlaka yako yanakuwa hayana tija, ya nini! Hatuwezi kubaki kwenye mamlaka kama mamlaka hayo hayaisaidii Serikali kutekeleza wajibu wake na kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda niwakumbushe wenzangu Kambi ya Upinzani, marafiki zangu kwamba, kama kuna sababu za msingi Bunge hili linaweza kuitisha taarifa yoyote toka Wizara yoyote wakati wowote. Mamlaka hiyo ipo na itaendelea kuwepo na mabadiliko haya hayaendi kuondoa hayo mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuu sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Riziki Shahali Mngwali ajiande.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana

wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2017 ambao kimsingi unafanya marekebisho kwenye Sheria ya Bajeti na kwenye Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme nakubaliana kabisa na mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali kwenye Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba sikubaliani kabisa na mawazo yaliyomo kwenye taarifa ya Kambi ya Upinzani ambayo yanasema Muswada huu unakwenda kunyang'anya mamlaka ya Bunge, sikubaliani kabisa na hilo na badala yake mimi naona kwamba Muswada huu unakwenda kuhakikisha kwamba, sasa Bunge linapolekwa taarifa, linaletwa taarifa ambayo ni rasmi na hivyo linafanya maamuzi *based on* taarifa ambayo ni rasmi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Serikali kwenye mambo ya muhimu kama Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Taarifa ya Uhamisho wa Fedha, Taarifa ya Matumizi ya Kila Kasma, *Compliance Report*, Taarifa ya Misamaha ya Kodi, hizi ni taarifa rasmi za Kiserikali ambazo ili itwe taarifa rasmi ya Kiserikali ni lazima iwe imepita kwenye *process* kadhaa. Wizara ya Fedha kazi yake ni *ku-compile* taarifa hizi zote nilizozisema kutoka kwenye taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Halmashauri na Mashirika mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *ku-compile*, Wizara ya Fedha inapitisha kwenye hatua nyingine ikiwepo *Inter-Ministerial Technical Committee* ambayo na yenyewe inapitia taarifa hizi na kuzihakiki na baadaye kuzithibitisha na badaye taarifa hizi zinakwenda mpaka kwenye *Cabinet* na kwenye *Cabinet* nako inahakikiwa na kupitishwa. Sasa

process hii ya taratibu zote hizi za Kiserikali hufanyika kila baada ya miezi sita ndio maana kuna *mid year review*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mapendekezo haya yanataka kuhakikisha kwamba taarifa zitazokuwa zinaletwa hapa na Serikali zitakuwa ni taarifa ambazo zimepita *process* zote hizi za Serikali mpaka *approval* ya *Cabinet* na hivyo kuwa taarifa ambazo ni rasmi na ambazo taasisi nyeti kama Bunge inafaa kuletewa na kufanya maamuzi. Ni kwamba sitegemei kama kuliletea Bunge taarifa ambazo ni *interim*, taarifa ambazo ni awali, taarifa ambazo hazijapita *process* hizi, eti ndio kulipa Bunge mamlaka. Kwa hiyo, sikubaliani kabisa na hoja iliyoletwa na Upinzani kwamba jambo hili litapunguza mamlaka ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mhagama, amesema wakati anachangia, ni kwamba Muswada huu hauzuii Kamati ya Bajeti au Bunge wakati wowote ule litakapona inafaa kuitisha taarifa yoyote kutoka Serikalini ambayo itakuwa ni taarifa ya awali kwa ajili ya kufanya mapitio au kufanya maamuzi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mahali popote kwenye Muswada huu ambapo Muswada umesema Kamati ya Bajeti imezuiliwa kabisa au Bunge limezuiliwa kabisa kuitisha taarifa ambayo Bunge litaonakwamba, inafaa kuitisha kwa wakati huo, hata kama iko kwenye hatua za awali, ili kufanya baadhi ya maamuzi ambayo yataonekana yanafaa kwa hiyo, Muswada huu hauzuii kwa hiyo, hakuna hofu yoyote ya kusema kwamba eti mamlaka ya Bunge yanapunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na mapendekezo ambayo tumetoa kwenye Kamati ambayo yanataka kwamba, mtumishi yeyote wa umma atakayepatikana kwamba, amekiuka Masharti ya Sheria ya Bajeti, basi aweze kupewa adhabu. Muswada umependekeza kukatwa mishahara ya miezi sita, lakini kuwa *subjected* na hatua za kinidhamu za Sheria ya Utumishi wa Umma, lakini sisi tumependekeza kwamba, mtumishi wa namna hii aongezewe pia tuhuma za kijinai kwamba kwa kukiuka masharti ya bajeti basi haitoshi tu kumkata mshahara wa miezi sita, bali akatwe mshahara wa miezi sita, awe *subjected* kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, lakini *in addition to that* vile vile apelekwe kwenye tuhuma za kijinai. Hili ni pendekezo ambalo tumelipendekeza kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Muswada huu maudhui yake makuu ni kuongeza ufanisi wa Serikali lakini kuhakikisha kwamba Bunge linaletewa taarifa za Serikali ambazo ni rasmi ambazo zimepita hatua zote za uandaaji wa taarifa hiyo na zimepata *approval* zote kutoka za Wizara *Interministerial Technical Committee* mpaka na *Cabinet* yenyewe. Kwa hiyo, taarifa itakayokuwa inakuja kila baada ya miezi sita ni taarifa ambayo ni *complete*, imejaa *facts*, ni taarifa rasmi na ambayo itafanya unyeti wa Bunge sasa uonekane kwamba ni chombo ambacho kinaletewa taarifa ambayo kwa kweli ni taarifa ambayo tunaweza kuiita taarifa kamili ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Waitara atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali na Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

MHE. MWITA M.WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye hoja hii ambayo imeletwa na Serikali. Nianze tu kwa kusema umeanza mtindo na naona umezoeleka na Wabunge wa

CCM. Tunapokuwa tunatoa hoja zetu kama Kambi ya Upinzani Bungeni tunatarajia aliyetoa hoja wakati wa majumuisho ndiyo azijibu hizo hoja, lakini Wabunge wa CCM muda wote wanajikita sana kupinga kile kilicholetwa hapa mezani. Wamejigeuza kuwa wasemaji wa Serikali na kwa hiyo sasa unashindwa kutenganisha mchango ambao umetolewa na Wabunge wa CCM na majibu ya Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mawaziri wanashindwa kufanya kazi yao vizuri. Tunatarajia, tunaomba Naibu Spika uongoze watu vizuri kwamba kama tumetoa hoja, tsubiri Mheshimiwa Waziri, huyu Mbunge wa CCM aliyepewa fursa kama hana neno la kusema akae kimya au akae chini na asuburi Waziri mwenye dhamana au Mwanasheria Mkuu wa Serikali...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara kuna taarifa.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kwa mzungumzaji ni kwamba, Mbunge aliyeko Bungeni hapa, anayo mawazo sahihi anayoona yanafaa kuzungumza katika Bunge hili siyo kwa kufuata chama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MWITA M. WAITARA: Huyu ndugu yangu wa Bunda naona sasa anaanza kukengeuka mimi sijasema...

NAIBU SPIKA: Sawa, sasa hebu Mheshimiwa Mwita Watara kaa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge tunasema kila siku humu ndani, Serikali iliyoko madarakani ni ya Chama cha Mapinduzi. Ndiyo maana inafika mahali Mbunge ukihojiwa mahali unasema kwamba Wabunge wengine wanasema ndiyo, ni kwa kuwa Serikali ni ya kwao. Sasa tusifike mahali tukaanza kuvutana kwa mambo hayo humu ndani Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Bobali amesoma kwa niaba ya Mheshimiwa Tundu Lissu taarifa ambayo wewe mchango wako naamini utaendana na hiyo. Yule kule utaendana na wa Kamati na utaendana na wa Serikali. Kwa hiyo, tusiende huko, Mheshimiwa Waitara, hawa Wabunge wana namna yao waachie chama chao, huku mna namna yenu, wewe endelea na michango yako hawa Wabunge hata ukiwaambia mpaka kesho Serikali ni ya kwao, wao watachangia mambo ya Serikali. Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

MHE. MWITA M.WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu ulindwe, lakini niseme tu kwamba kwa sababu hiyo kwa sababu Spika wa Bunge hili ni wa Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo maamuzi yote ambayo mnatoa ni ya CCM na wewe Naibu Spika hata mwongozo ulioutoa unatoa ni wa Ki-CCM...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, Waitara, Waheshimiwa Wabunge msilazimishe kufanya mambo ambayo hayapo, msilazimishe Kiti hapa, ndiyo maana kimekupa wewe nafasi na siyo Mbunge wa CCM, kwa hiyo usifike mahali ukaanza kuona Kiti kinafanya maamuzi kwa namna ya CCM. Mimi nimetokana na Chama cha Mapinduzi, ndiyo, lakini kanuni zinanitaka na wewe nikupe nafasi kama nilivyowapa hawa. Wewe ni wa Chama cha Mapinduzi unapopewa nafasi ya kuzungumza humu ndani? Mambo ya vyama Waheshimiwa tuyaache kwenye vyama.

Kama jana, vyama vyote vilikuwa na *caucus* kila watu wamejadili wanayoona inafaa. Tusiende huko Waheshimiwa tafadhali, kila chama kilileta hapa wagombea, wagombea kadhaa wakashinda wengine wakashindwa. Tusianze huo mjadala hapa ndani. Mheshimiwa Waitara changia hoja iliyo mbele yetu hapa, tafadhali.

MHE. MWITA M.WAITARA ... Mheshimiwa Naibu Spika, nakuheshimu sana na naomba niseme habari ya vyama ianze na Kiti.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara naomba ukae chini. Mheshimiwa Shahari mchango wako.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: *Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi aliyetupa afya na uzima sisi zote tuliomo humu na nazidi kumwomba ajalie kikao hiki kifupi kitoke na maamuzi ya busara kwa ajili ya maslahi mapana na ya muda mrefu wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala tunalojadili hapa ni muhimu kama ambavyo tumejadili mengine na sidhani kama nitakuwa na maneno tofauti sana ya kusema mbele yako, bali kurejea yale kwamba tumche Mwenyezi Mungu kwa namna ya kumcha na katika imani yangu tumefundishwa kukumbushana kwamba kukumbusha hakika kunawasaidia wenye kuamini na nawakumbusha Waheshimiwa wote mliomo humu kwamba tumwogope Mwenyezi Mungu, tutunze viapo vyetu na naamini ninyi ni waumini, kwa hiyo ukumbusho huu utawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, nilikuwa nashangaa hapa nikimwangalia *prince* wangu wa Madaba Mheshimiwa Mhagama, nikimwangalia na *prince* Mheshimiwa Rashid Shangazi wanashangilia nasema wamebadilika lini, nilikuwa najiuliza mwenyewe hapa, wamebadilika lini? Kwa sababu siku ambayo Waziri husika alikuja kwenye Kamati, hakuwa na hoja za msingi, kabisa. Mwisho tukamwambia kwa hali tuliyonayo sasa hivi kwa namna *technology* ipofikia hata tukikwambia utuletee *report monthly, weekly*, hutaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hakuna sababu ya msingi hoja ya maana kwamba eti sasa mkileta ripoti baada ya miezi sita itakuwa ya maana zaidi kuliko ya miezi mitatu, si kweli. Naomba Mwenyezi Mungu nishuhudie nasema si kweli. Utaratibu tuliouweka mwanzo ndiyo

unawezesha hiki ambacho kimesemwa hapa kwenye taarifa ya Kamati yangu kwamba marekebisho hayo yaongeze uwezo wa Bunge kugundua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utagunduaje haraka wakati muda wenyewe umeshauweka mrefu? Vipaumbele ambavyo havijatekelezwa matumizi yasiyo na tija, vyanzo vya mapato visivyofanya kazi vizuri. Umshaondoa ule muda wawewe kukufanya ukagundua hilo haraka, ambao ni miezi mitatu unasema ukae mpaka miezi sita haraka iko wapi Waheshimiwa. Waheshimiwa haraka iko wapi unapotoka kufanya kazi miezi mitatu, useme tsubiri mpaka miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii si haki, narudia tena, si haki, Waheshimiwa tuiheshimu nchi hii, tuwaheshimu wananchi waliotuweka huku na tuweke maamuzi na tufanye kazi hii kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii, hayo marekebisho hasa hayo yanayobadilishwa kwamba utoaji wa taarifa hizi kwa kweli si wa haki. Si wa haki hata kidogo na tusijidanganye hapa hicho ulichokisema Mheshimiwa Naibu Spika kwamba tuache vyama nje ni kweli tuache vyama nje, hapa tuwaangalie Watanzania, hapa tuangalie Serikali yetu, hapa tuangalie mamlaka yetu Bunge ni vipi tunaweza kutekeleza mamlaka hayo, vipi tunaweza kutekeleza majukumu hayo kwenye mazingira ambayo kweli yanawezesha hilo. Mimi wala sitajali hata nikiambiwa Bunge tutakutana mara moja kwa mwaka, lakini muhimu yale majukumu yetu ya Bunge tuyafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, tunaliua Taifa hili, tunajenga uzembe katika utendaji kazi wa Serikali kwamba mkae tu tusiwakague, mkae tu tusiwakague kwa miezi sita, maana yake ripoti itakuwa inatoka mara moja tu. Kwa sababu *by the time mid year* ya pili inakamilika mwaka mwingine umeshakamilika, *whether* uwe mwaka wa kifedha au mwaka wa kalenda, jamani tunakwenda wapi au tunaipeleka wapi nchi hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na yaliyoletwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba hii Serikali tubaki pale pale kwenye kuletewa taarifa kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa Kiongozi wa Cuba aliwahi kusema wakati wa yale mapinduzi makubwa ya 1950s kwamba *condemn me I don't care history shall observe me*. Semeni mtakayosema lakini ukweli utabaki kuwa ukweli. Tuiteni majina; tuiteni nyati, tumbili, kobe *whatever the name you like to call us*, lakini ukweli utabaki kuwa ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanangu Kafullila alitwa majina hapa wakati wa Escrow, *Escrow* iko wapi sasa hivi, ukweli utabaki kuwa ukweli kwa sababu ukweli ndiyo kauli ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mwadilifu, kwa hiyo kauli hata siku moja haitokwenda vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sina maneno hata kama muda bado upo lakini ni lile lile kwamba turudi pale pale tulipo tuletewe ripoti kila baada ya miezi mitatu, lakini muhimu zaidi tumwogope Mwenyezi Mungu na tutunze viapo vyetu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Riziki. Mheshimiwa Joram Hongoli, atafutiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta Muswada huu sasa baada ya kuona kama alivyosema msemaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Mhagama, baada ya kufanya tathmini kuona kwamba *practically* utaratibu wa zamani hauleti tija, basi ameamua kuja na marekebisho haya ili tuweze kuisaidia Serikali na Wizara iweze kuwa na tija katika kutoa taarifa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashangae baadhi ya Wajumbe wa Kamati hasa upande ule wanaolalamika juu ya Muswada huu. Tumefanya kazi wote na Waziri amekuja na maelezo mazuri na Mwanasheria Mkuu ametoa ufafanuzi mzuri, Kamati tukaelewa, tukaona umuhimu wa kukubaliana na marekebisho au kukubaliana na haya maombi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshangaa dada yetu pale, mama yetu Riziki. Ndiyo matatizo ya kuwa mtoro kwenye Kamati, ungekuwepo jana ungepata taarifa vizuri. Kwa hiyo, nikubaliane na Muswada huu, ni utaratibu wa kawaida popote pale kwa Serikali zote duniani, marekebisho ya baadhi ya Sheria kama tunavyosema kwamba ni *progressive process* kwa hiyo kilichofanyika...

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Riziki Mngwali.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba, mimi siyo mtoro na hata jana ambayo sikuwa kwenye kikao cha Kamati nilimjulisha Katibu, lakini kama hivyo ni kweli basi atoe jina langu humo kwenye hii taarifa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli unaipokea taarifa hiyo?

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa kwa sababu kikao cha jana kilikuwa ni muhimu sana kwetu Wanakamati na ndiyo maana tumekuja na msimamo huu kama Kamati kwa sababu yale yaliyoletwa jana na Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo iliyotujengea tuweze kuamini kwamba huu Muswada ni wa muhimu kuupitisha, kwa hiyo ndugu yangu hukuwepo basi ndiyo maana mambo yamekupita. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaona hata kwenye halmashauri zetu taarifa zetu, kama huwa mnahudhuria vikao

Waheshimiwa Wabunge mnaweza mkajifunza tu kwenye halmashauri, kwenye halmashauri Kamati za Fedha na Mipango zinakaa kila baada ya miezi mitatu mitatu, unaweza ukajifunza jinsi gani taarifa zile zilivyo, unakuta zina matatizo mengi. Sasa je, katika *National Level* kwa maana ya Wizara na Wizara hizi zinategemea kupata taarifa hizi kwenye taasisi mbalimbali za Serikali, mojawapo ikiwa ni halmashauri, kunakuwa na matatizo makubwa. Kwa hiyo, ni kweli kabisa Serikali isingeweza kufanya majukumu yake vizuri na wasingeweza kuja kuwa na taarifa nzuri kama sehemu ambazo wanategemea kupata taarifa hizi kama taarifa za mapato na matumizi, zinakuwa siyo *realistic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipongeze Wizara kwa kuja na utaratibu huu wa miezi sita, kuna uhakika kwamba Serikali itakuwa na muda wa kutosha wa kufanya kazi. Itafanya kazi angalau miezi mitano na ule mwezi mmoja wata-*complied* taarifa na sisi Wabunge tutapata taarifa ambazo zimekuwa *realistic*, taarifa ambazo ni za uhalisia. Kwa hiyo, hiyo ni moja ya faida ambayo tutaipata kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni utaratibu wa makampuni mengi makubwa, makampuni ya kimataifa, lakini ni utaratibu hata wa nchi nyingine, Wabunge wengi mmezunguka nchi mbalimbali, kama mmewahi kukutana na Mawaziri au kujifunza taratibu za uwasilishaji wa bajeti, utakuta mara nyingi wanawasilisha mara mbili kwa mwaka. Kwa hiyo na sisi tunajifunza *which are the best practices* toka kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo hii itasaidia pia kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaweza ikatoa taarifa vizuri, taarifa ambazo hazina walakini, taarifa ambazo hazina upungufu, kwa hiyo nami pia naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni gharama, Waziri amekuwa akichapisha vitabu hapa vinajaa pale kwenye *Pigeonholes* zetu, hatusomi wakati mwingine, lakini tukiwa na taarifa mbili, vitabu viwili tunakuwa na muda wa kusoma vizuri. Vile vile tunapunguza gharama kwa Serikali ya kuchapicha vitabu. Pia tutapunguza gharama ya muda

ambao watumishi wetu wa Serikali wanakaa kwa ajili ya kuandaa taarifa, kila baada ya miezi mitatu wanaandaa taarifa. Ni gharama ya muda, lakini pia *financial cost*, kuna *financial cost implication* pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba naunga mkono hoja kwa utaratibu huu ili tuweze ku-save gharama ya muda lakini pia tuweze ku-save gharama za kuchapisha vitabu. Vilevile niunge pia mkono kwa hii sheria kutaja ni nini kitafanyika kwa afisa yeyote ambaye hatatekeleza majukumu yake vizuri maana yake hapa ungeweza kutokea uzembe. Kwa hiyo, niunge mkono kwamba Sheria imesema vizuri kwamba huyu Afisa atakatwa mshahara wake wa miezi sita, lakini pia na taratibu nyingine za kijinai zitachukuliwa. Hii itawafanya pia watumishi wetu ambao wana jukumu la kuandaa taarifa waweze kuwa makini katika uandaaji wa taarifa na wahakikishe kwamba wana-*meet deadline* iliyotolewa na Wizara kuwasilisha taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naomba Sheria iweze kupitishwa vizuri ili ianze kufanya kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi na Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuata.

MHE. RICHARD P.P MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kuwasilisha mabadiliko haya ya Sheria ya Bajeti pamoja na ya Ofisi yake. Naomba Wabunge kwanza tujjulize hizi taarifa ya utekelezaji ni kwa ajili ya nani, zina manufaa gani katika shughuli zetu za Kibunge. Unapopata taarifa yoyote, *performance report* unaangalia na aina ya taasisi ambayo inatoa hiyo ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwa upande wa Serikali, Serikali siyo kampuni inayofanya biashara, iko kwenye ushindani kwamba inahitaji ipate *daily, weekly, monthly or*

quarterly reports kwa ajili ya kufanya maamuzi ili kuboresha biashara wasitoke katika ushindani, Serikali haiko hivyo. Serikali shughuli zake zimenyooka, zinaeleweka, vyanzo vya mapato haishindani na watu wengine. Kwa hiyo, kubadilisha hii Sheria kutoka miezi mitatu mpaka miezi sita kwa ajili ya kupata taarifa ya utekelezaji maamuzi waliyofanya ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hizi ripoti zinatusaidia katika kufanya maamuzi ya mbeleni, katika kupanga mipango. Vyote vinatusaidia, pia katika kudhibiti. Hata hivyo, tunayo mikakati na Serikali inafanya kazi kila siku. Tuna Baraza la Mawaziri lina vikao vyake, tuna Baraza la Kazi lina vikao vyake, tuna Watendaji Makatibu Wakuu katika Idara, katika Wizara mbalimbali wana vikao vyao vya ufuatiliaji, kwa hiyo suala la kufuatilia utekelezaji upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge wamezungumzia kuhusu halmashauri kwamba Kamati ya Fedha na Mipango zinakaa kila baada ya miezi mitatu, lakini halmashauri zingine zinakaa kila mwezi zinapitia mapato na matumizi ya kila mwezi na kushauri nini kifanyike. Kwa hiyo, ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali upo kuanzia ngazi ya Serikali Kuu mpaka kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala limezungumzwa na wenzangu wa Upinzani kwamba kubadilisha hii sheria tunakwenda kupunguza mamlaka ya Bunge, hiyo sio sahihi. Tuko kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63, tunaisimamia na kuishauri Serikali na tutaendelea hivyo hivyo. Kanuni zetu, kazi za Kamati kwa mujibu wa Katiba tutaendelea nazo kwenye vikao vyetu taasisi mbalimbali zitaendelea kuleta ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukifuata sheria mbalimbali ambazo tumepitisha kwa taasisi zilizopo, zinafunga mahesabu mwezi Juni, wanapewa miezi mitatu kuandaa hizo ripoti, kwa hiyo Septemba 30 wanawasilisha. Baada ya hapo zinakwenda kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Serikali na yeye atapeleka kwa Waziri husika, Waziri husika ataleta kwenye Bunge kwa kupitia hizo Kamati; hizo sheria

zingine hatujazigusa. Kwa hiyo, madaraka ya Bunge bado yapo pale pale tofauti na Kambi ya Upinzani wanavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwamba tumeahidi kwenye mikutano fedha nyingi ndiyo maana tunabadilisha, hela tunapeleka kwenye ndege, sio sahihi. Tulichokiahidi ndicho ambacho tunaendelea kutekeleza na mkiangalia wakati kila Wizara ambayo imesoma bajeti yake hapa, ilieleza utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017, mfano tu Wizara ya Nishati na Madini walitekeleza kwa asilimia 52 mpaka kufikia mwezi Machi. Sasa nini ambacho kimefanyika ni kwamba utekelezaji bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupata misaada na mikopo; nchi nyingi kupata misaada na mikopo ni pamoja na masharti ambayo unayatimiza na mkiangalia taarifa ya ripoti ya Wizara ya Fedha wakati bajeti inasomwa, tumepata mikopo mingi mwezi Juni na Mei na mpaka Juni hapo Waziri wa Fedha anasema tumepata mkopo wa dola milioni 500 kutoka India. Kwa hiyo, yote haya ni mambo ambayo yataingia kwenye taarifa ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kubadilisha hii sio kwamba tunaenda kupunguza ufanisi, hatupunguzi, ufanisi utabaki pale pale na Bunge tutaendelea kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja imegusiwa kwamba muda ni mrefu. Suala la muda halina tija, suala ni kuangalia. Unaweza ukaletewa ripoti kila mwezi, lakini je mfumo uliopo unadhibiti watu kufanya kwa ufanisi? Kwa hiyo, unaweza ukapewa kila siku ripoti au baada ya miezi mitatu lakini je mfumo uliopo unadhibiti kufanya kazi kwa ufanisi, hilo nalo la kuangalia. Kwa hiyo, tusiangalie tu ripoti lazima tuangalie na mfumo na ndio maana sasa hivi mnasifia uongozi uliopo kwamba unafuatilia, nayo ni mambo ambayo mtaona kwamba yanasaidia kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imeonekana hapa kama vile CAG anapunguziwa majukumu. Hakuna sheria

yoyote ambayo imebadilishwa hapa kwamba CAG ataenda kupunguziwa majukumu katika utekelezaji wake wa kazi za kila siku; CAG atabaki pale pale. Atakuwa anatekeleza na anaripoti kwenye Bunge na sehemu zote zinazohusika na wengi kama mchangiaji Hongoli alivyosema, tunapewa vitabu kibao na leo wengi tutaondoka na vitabu hapa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

T A A R I F A

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimpe taarifa mwongeeaji anayeongea kwamba inatakiwa tu afahamu kwamba sisi tuliopo huku kazi yetu ni kuishauri na kuisimamia Serikali na nyie huko kazi yenu ni kuipongeza Serikali na kuitetea Serikali. Kwa hiyo, lazima muone hiyo tofauti, sisi kazi yetu ni kuishauri na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka inavyoonekana kwenye Kamati lazima idadi yenu ni kubwa sana kama kamati zinakuja na mawazo haya, lazima ninyi idadi yenu ni kubwa sana kwenye Kamati. Mheshimiwa Richard Mbogo unaipokea hiyo taarifa?

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba kaka yangu Zuberi Kuchauka ananifahamu vizuri, sikutegemea atoe taarifa kama hiyo. Ni kwamba Wabunge wote tunafanya kazi kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2) kuisimamia na kuishauri Serikali na majukumu mengine tunafanya kupitia Kamati. Kwa hiyo, taarifa yake sio sahihi, kilicho kizuri kwa Serikali tutapongeza na mahali ambapo wanakosea huwa vile vile tunashauri na tunakosoa na mimi ananielewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba mabadiliko ya sheria hii sio mabaya kama wanavyodhani na kama wanavyofikiria. Suala kwamba CAG

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tulimpa bajeti ndogo sio sahihi, bajeti alipewa na Serikali iliahidi kwamba ataongezewa na aliongezewa na bajeti hii kama alivyoileta bilioni 12 za *World Bank* na zingine zimetoka Serikalini karibuni bilioni 60, kwa hiyo ana bilioni sabini na kitu. Kwa hiyo, bajeti ya *CAG* iko vizuri, kwa hiyo sio kwamba tume-*impair independence* yake kwa kufanya kwamba tunampa bajeti ndogo, hilo lazima walielewe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia tu naomba niseme kwamba sio rahisi kupata taarifa kwa wakati kwa sababu taarifa zingine tunapata kutoka taasisi binafsi ambao hawatoi ushirikiano kwa Serikali. Kwa mfano, suala la takwimu, ukisema leo hii unaandaa pato la Taifa, unaandaa taarifa sio za Serikali tu, mpaka taasisi binafsi lazima upate takwimu zao na mauzo yao ili uweze kujua kwamba pato la Taifa likoje. Sasa watu wetu wa *NBS (National Bureau of Statistics)* wakifuatilia kwenye taasisi za binafsi wanapata shida kwenye kupata takwimu, watu hawafanyi *declaration* kwa hiyo ni jambo linalochukua muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kuomba miezi sita lipo sahihi na bado kimfumo wa kiteknolojia hatujaunganishwa vizuri; tuna *EPICAR* mfumo wa uhasibu, bado sehemu zingine haujakamilika, kuna Halmashauri mpya bado hazijakamilika. Kwa hiyo kiteknolojia bado, lakini Serikali bado inaendelea na jitihada. Kwa hiyo, lazima waelewe kwamba suala la miezi sita sio kwamba Serikali imekurupuka, imeangalia maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi tutamalizia na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ili niweze kutoa mawazo yangu na mchango wangu katika marekebisho ya Sheria ya Bajeti hasa kwenye vifungu ambavyo vinaenda kuleta marekebisho

kwenye *reporting* kutoka *quarter* kwenda kila baada ya miezi sita kama taarifa za matumizi, utekelezaji na taarifa za mapato na matumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kwenye kuchangia hoja yangu kwa kuunga mkono hoja/maoni yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Nitaanza kwanza na ushauri ili tujue tunaendaje endaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeona tuna changamoto tunashindwa ku-*deliver quarterly*, hatuna haja ya kubadili sheria, tuongeze muda bali inabidi tuangalie kwenye *system* zetu tufanyeje kazi ili tuweze ku-*improve performance*. Kama ni mambo ya *software* ama mfumo wa *reporting* una kasoro basi huo ufanyiwe marekebisho na sio sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Tanzania ni wajumbe wa *Commonwealth*, sasa ni Mabunge yapi katika *Commonwealth countries* zinaenda ku-*report* kwa kutumia kila baada ya miezi sita na sio *quarterly*. Kwa nini sisi tunataka kuwa wa tofauti na ni sababu gani nzito zinazotaka kufanya sisi tubadilisha mfumo wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Bungeni hapa tunakutana mara nne kwa mwaka kwenye Kamati zile tendaji ili tuweze kuisimamia Serikali na kushauri *otherwise* pale tunapotakiwa kushauri. Sasa tunapokutana kwenye Kamati tunaletewa taasisi ama Wizara mbalimbali za Serikali zinaelezea utekelezaji wao, tunazichunguza utekelezaji wao; sasa ule utekelezaji tunaupimaje bila kuangalia matumizi yalikuwaje na *sources* za mapato zilikuwaje. *How are you going to analyze* bila ripoti ya mapato na matumizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni hivi; mfumo wa *quarterly reporting* haujashuka tu, kuna *benefits* zake; ndio kuna changamoto zake lakini *benefits* naona zipo nyingi kuliko upungufu wa kuripoti *quarterly*. Tunavyopanga mipango yetu, tunataka kupitisha bajeti ya mwaka, ile *budgeting* imekuwa *shaped* na tulichokipanga kwa mwaka

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

huo. Sasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunapimaje miezi sita *half a through*, mwezi wa Saba, Nane, Tisa, Kumi, Kumi na Moja na Kumi na Mbili ndio uangalie kuna shida gani? Hapo tayari tumebakiza miezi sita tu inayobaki, sio rahisi kufanya *rectification* zozote kama kuna upungufu mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi kuboresha utendaji wa progamu au malengo au shughuli za kiutendaji kwa kusubiri mwisho wa mwaka au karibuni nusu mwaka. Kipimo kizuri cha utendaji na ndio tunachokifanya, si tunalipana mishahara kila mwisho wa mwezi, Ofisi si zinatakiwa zilipe *bills* kila mwisho wa mwezi, kwa hiyo kuna *accounting system* ambayo kila mwisho wa mwezi inafanya *checks and balances*. Sasa shida iko wapi ku-*compile* kila mwezi ukaripoti miezi mitatu mitatu. Kwa nini usubiri miezi sita? Hapo hatuoni kama tunaweka *loophole* ya kufanya yasiyotakiwa kwenye utendaji wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *system ya quarterly* pia inasaidia kuboresha uwazi na kuongeza umahiri; yule kama ni *Accounting Officer au Program Officer* unampa muda, miezi sita; wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano na wa Sita na zile ripoti anazo kila mwezi anatakiwa afanyie kazi; hapo tunaipa nafasi ya kulega lega na kutokuweka udhibiti thabiti wa kusimamia mapato na matumizi. Ni bora ujue tatizo liko wapi mwanzoni kuliko kusubiri miezi kadhaa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna umuhimu wa kuboresha udhibiti juu ya taarifa za fedha ambao *at least quarterly* ulikuwa unatupa mwangaza na sisi Waheshimiwa Wabunge tunapokutana kila Kamati, hii ilikuwa inatupa uwezo wa kufanya kazi zetu vizuri. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umwekwisha. Mheshimiwa Rashid Shangazi atakapomaliza,

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali utakuja kuhitimisha hoja.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kupata fursa hii. Nianze na maneno matakatifu aliyoyasema Nabii Issa au baba yetu Yesu wakati yupo msalabani pale alisema baba wasamehe kwa sababu hawajui wanalolitenda. Nami naomba niwasamehe *Kambi Rasmi ya Upotoshaji Bungeni wala sina sababu ya kumjibu yeyote. (Makofi/Kicheko)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabudi jana alitupa somo zuri sana kwamba mkubwa akikosea basi unamuacha tu kama alivyo...

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi kuna kuhusu utaratibu, kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1) inakataza Waheshimiwa Wabunge kutumia maneno ya kuudhi na maneno ya matusi na lugha zisizostahili zisizokuwa za kibunge; hakuna Kambi ya Upotoshaji Bungeni na wewe unafahamu. Kwa hiyo, namwomba afute maneno hayo na aendelee na mjadala wake kistaarabu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Shangazi, hakuna Kambi ya Upotoshaji Bungeni kwa hiyo neno upotoshaji weka neno linalohusika hapo.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; naomba isomeke Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lakini wapo wapotoshaji ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu...

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Sheria hii ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu...

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi, kuhusu utaratibu kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kanuni hiyo ya 64; utaratibu ulioombwa na Mheshimiwa Mtolea ni kwamba Mheshimiwa Mbunge afute kauli ya neno upotoshaji, lakini anafuta huku anaongeza lakini wapo wapotoshaji. Kwa hiyo bado hajafuta hilo neno; kwa hiyo naomba ufute. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Maneno upotoshaji huwa mnayatumia Wabunge siku zote humu ndani kwamba, fulani kapotosha, huwa hamuombi yafutwe. Ndio maana nimesema kwa kuwa ameita Kambi ya Upotoshaji Bungeni aite sawasawa, ndicho nilichosema hapa au wewe umenisikia vipi? Nimesema afute ili aite kambi kwa jina halisi lakini maneno ya upotoshaji mnayatumia; mbona nyie huwa mnawaambia Mawaziri hapa wanapotosha, kwani kuna mtu amewahi kusema afute neno?

Naomba ukae Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Shangazi ameshaondoa neno upotoshaji kwenye jina halisi la Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba niendeele. Ni kweli kama alivyosema mama yangu Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, mwanzoni tulikuwa hatukuelewa vizuri hii sheria ambayo imeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, lakini kadri tulivyokuwa tunaendelea Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri mwenye dhamana wamekuja kutoa somo katika Kamati yetu na imefika mahali bila unafiki tunasimama hapa tukiwa na

mind nzuri kabisa tukiamini kwamba, sheria hii inakwenda kufanya kazi ambayo ndiyo mara nyingi tunailalamikia hata humu Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge karibu wote hapa huwa tunalalamika kila siku kwamba bajeti ya Serikali sio *realistic*, kwa nini tunaweka *projection* kubwa lakini mapato yanakuwa madogo; kwa sababu ni makisio na haya makisio yanaanza kufanywa katika Halmashauri zetu. Halmashauri inafanya makisio ndani ya miezi mitatu inapeleka kunako husika na mwisho wa siku wanapokusanya mapato halisi yanapishana na yale makisio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili tutengeneze utaratibu na kuwa na mwanzo mzuri wa *realistic budget* ni lazima sasa tuipe Serikali muda mrefu wa kuanza kukusanya na kuleta ripoti baada ya miezi sita. Huu wala sio utaratibu mgeni, ni utaratibu ambao *hata South Korea* wanautumia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kabisa katika vyanzo vyetu vya mapato kwenye Halmashauri nyingine vinategemea zaidi mazao, upo wakati kati ya mwezi mmoja hadi mitatu unakuta Halmashauri fulani haina mazao yoyote. Kwa hiyo, utarajie kwamba kwa kipindi hicho Halmashauri hii haitakusanya chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, Mheshimiwa Mwita waitara kule Jimboni kwake wengi ni wafugaji wa kuku, sio kwamba akishaanza kuku pale dakika hiyo hiyo atapata mayai; ni baada ya muda fulani mayai yatapatikana labda ndani ya wiki mbili au tatu na kama kuna ushuru ndio ataanza kulipa. Kwa hiyo, hizi *projections* zote zinakwenda kuwekwa kwenye maduhuli ya Serikali na vyanzo mbalimbali vinavyotokana na mapato ambayo sio ya kodi kama kwenye mahakama na kadhalika. Kwa hiyo, ndani ya miezi sita ndio tupate ripoti. Hizi ripoti ambazo tunapata sasa hivi ndani ya miezi mitatu ni ripoti ambazo ni *premature* kwa sababu hazina *approval* ya Baraza la Mawaziri, lakini hii ya miezi sita inakwenda kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hebu tuone kwa *concern* hiyo. Tusiende mbali kusema kwamba Bunge linanyang'anywa madaraka yake; madaraka ya Bunge yapo kimsingi kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) yapo wazi kabisa yamewekwa pale, lakini pia tunakutana katika Mabunge manne na kila Bunge hapa lina kazi yake Waheshimiwa Wabunge. Bunge hili tulilokula nalo ni kwa ajili ya kupitisha bajeti ya Serikali; Bunge la mwezi wa Tisa tukija hapa ni kwa ajili ya kutunga sheria ndio muktadha; la mwezi wa Kumi na Moja lile ni la uchunguzi na kupokea ripoti za CAG, LAAC na kadhalika na mwezi wa Tatu ni *oversight* na hii *oversight* ndiyo hizi pesa ambazo tunapeleka mwezi wa Tatu ndio tunaenda kuziangalia zimefanyaje kazi, tunakwenda kuisimamia Serikali pale imetekeleza vipi. Kwa hiyo, ninaposema upotoshaji ndio hili ambalo namaanisha, kwa hiyo naamini kwa muktadha huo tutakuwa tumeelewana vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachozungumza hapa pia ni suala zima la kwamba kama nilivyotangulia kusema kwamba lengo mahususi ni kuhakikisha kwamba sasa Serikali inapata bajeti ambayo ni *realistic*, tusije hapa tukapendezeshana tu kwamba bajeti inasomwa lakini haiendeni na mapato tuliyokusanya. Pia hata mwaka jana mpaka Novemba Serikali ilikuwa bado haijapeleka pesa kwenye Halmashauri zetu na tukaja hapa tukalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukamlalamikia sana Waziri mwenye dhamana ya afya kwamba madawa hayapatikani, lakini chanzo chake ni hiki hiki tunachokisema kwamba hata sheria, tumebadilisha hapa *Finance Bill* na imeanza kufanya kazi tarehe moja, sio kwamba inapoanza kufanya kazi moja kwa moja kuna taratibu nyingine za kiofisi bado hazijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta Serikali mpaka ijipange tuanze kubadilisha majedwali na kadhalika mpaka mwezi wa 11 pesa bado hazijaingia kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tunapojadili mambo haya tuache kutumia akili za vikao vyetu vya pembeni pembeni, tujaribu kutumia akili za

kawaida kabisa kwa muktadha wa shughuli za Kibunge ili tuweze kuishauri na kuisimamia Serikali vile inavyopaswa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu ndio hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mtoa hoja.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana. Natambua uwezo mkubwa na umakini wa Wabunge hawa, ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kuisimamia na kuishauri Serikali inapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa namna ya pekee leo pia naomba kutambua sana uwezo mkubwa walionao Wabunge, muda hautoshi, nitawataja hawa waliopata fursa ya kuchangia ambao kwa elimu yao kubwa sana wamenisaidia hata mimi kuelewa mambo mengi na bila shaka Wabunge ambao walikuwa hawaelewi wameelewa mambo mengi ya msingi wa mabadiliko haya ya sheria. Naomba niwataje; Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Madaba; Mheshimiwa Zedi, Mbunge wa Bukene; Mheshimiwa Joram Hongoli, Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hawa wametoea elimu kubwa sana katika Bunge hili kuhusu umuhimu na maudhui ya Muswada huu. Naamini Waheshimiwa ambao walikuwa hawaelewi nao wamenufaika sana na elimu hii. Waheshimiwa hao ni pamoja na Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Riziki Shahari, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Sware, nadhani ni hao. Kwa hiyo nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wabunge hawa... (Makofi)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Na naomba kuendelea kusahihisha. Mchango mzuri na elimu nzuri waliyoitoa Waheshimiwa Wabunge hawa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuna kuhusu utaratibu, Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba ukae kidogo. Kanuni iliyovunjwa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ni namba 64(1)(a), inazungumza kwamba mzungumzaji, kaka yangu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atasema jambo ambalo lina ukweli. Sasa anapotaja kwamba mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao hawakuelewa sio kweli, mimi nilielewa na nina hoja kinzani juu ya hicho ambacho anakielezea yeye.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba uendelee.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, na pia namshukuru Mheshimiwa Waitara kwamba sasa ameelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo mazuri ya mchango wa Wabunge hawa ndani ya Bunge hili sitakuwa na mengi ya kusema. Isipokuwa kwa sababu nina wajibu wa Kikatiba wa kufafanua hoja hizi za kisheria; niseme tu kwamba, moja, Waheshimiwa Wabunge naomba kuwahakikishia, kama ambavyo baadhi ya Wabunge

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wamechangia, mabadiliko haya ya sheria hayakusudii kwa namna yoyote kupora au kupoka mamlaka ya Kikatiba na kisheria na Kikanuni ya Bunge hili kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ufanisi ipasavyo, inapokuwa inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu haya ya Kikatiba bila kurejea Katiba yameelezwa vizuri Ibara ya 63(2) na (3) kuwa Mbunge anaweza akamuuliza Waziri na Serikali jambo lolote lile linalohusu mambo ya Muungano, lakini ni vizuri niliseme kwa sababu nadhani muda utaweza kutosha ili wananchi nao wapate kulielewa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba hii inasema hivi, 63(2):

“Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.”

Mheshimiwa Naibu Spika, 63(3);

“Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza–

(a) kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya Umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake;”

Mheshimiwa Naibu Spika, haya hayategemei hizi ripoti za robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika 63(3);

(b) kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti;”

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wala sio Muswada wa kubadilisha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, wala sio Muswada unaobadilisha Kanuni za Bunge na Muswada huu haukubadilisha kabisa kifungu cha tisa (9) cha Sheria ya Bajeti ambayo bado mamlaka yake yamebaki pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tisa (9) cha Sheria ya Bajeti kinahusu madaraka ya Kamati ya Bajeti. Naomba niyasome madaraka haya ya Kamati ya Bajeti tuone kama yameguswa kwa mabadiliko haya. Kifungu cha 9(1) kinasema:

“The Parliamentary Budget Committee shall, in addition to functions provided under the Parliamentary Standing Orders, carry out the following functions:

- (a) discuss and review the Plan and Budget Guidelines, budget estimates and make recommendations to the National Assembly;*
- (b) consider the Budget and make recommendations to the the National Assembly;*
- (c) scrutinize the budget estimates of the National Audit Office, Judiciary and National Assembly;*
- (d) provide general recommendations to the National Assembly and Parliamentary Standing Committees on budgetary matters;*
- (e) monitor all budgetary matters falling within the powers of the National Assembly under this Act or any other law and report on those matters to the National Assembly;*
- (f) monitor adherence by the Government and public entities to the principles of public finance set out in the Constitution, other laws in force, and to the fiscal*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

responsibility principles set out in the Public Finance Act and this Act;

- (g) examine quarterly financial statements and other documents submitted to the National Assembly and make recommendations for improving the management and accountability in respect of public finances;*
- (h) conduct periodical study on the performance trend of the Budget and make recommendations to the National Assembly for improvements;*
- (i) do any other act or activities relating to budgetary matters as may be assigned to it by the National Assembly under this Act or any other written law; and*
- (j) in relation to oversight responsibility, discharge or perform any function as spelt out under the Parliamentary Standing Orders.*

(2) For the purpose of subsection (1), the Parliamentary Budget Office shall provide the Parliamentary Budget Committee with professional services in respect of budget, finance and economic matters."

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaona kabisa Waheshimiwa Wabunge mamlaka ya Kamati ya Bajeti hayakuguswa kabisa hata katika mapendekezo haya, wala hata mamlaka yake hayazungumzi hata *quarterly* ya ripoti ukiisoma hii, *it does not mention about quarterly reports*. Hata hivyo, wamepewa mamlaka, tena kwa wakati wote wapo pale. Yaani wao mamlaka yao pale wanaendelea kuangalia wakati wote *performance* ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba Waheshimiwa Wabunge mridhie mapendekezo haya ambayo yameletwa na Serikali. Kwa namna yoyote hayataathiri Mikutano ya Bunge, mikutano hiyo ni ya Kikatiba, ni ya kikanuni na mamlaka yenu ya kuisimamia Serikali

hayapokonywi na haya. Kwa hiyo, kwa mara nyingine tena niseme tu kwamba nimeridhika na kufarijika sana na mchango mzuri na elimu iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge hawa ambao nimeshawataja na ufafanuzi huu unatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri Bunge lako Tukufu liunge mkono hoja hii, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Toa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu unaofuata, nitawahoji baadaye. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017)*

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya neno *notice*, Serikali imeleta marekebisho kwa ku-*insert arrangements of sections*.

(Marekebisho yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta marekebisho kwa vifungu vingi, lakini kifungu cha nne (4) kinafanana na vifungu vingine na kulingana na mjadala uliopo humu ndani na maneno ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kwamba sisi hatuelewi na kuna wengine wanaelewa, naomba niondoe hoja zangu zote kwa sababu kunatokea ubaguzi kwenye Bunge hili wa kutukashifu Wabunge wengine kwamba hatuelewi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, Mheshimiwa Waitara ameondoa marekebisho yake yote, kwa hiyo tutaendelea. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 15

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja, taarifa. *(Makofi)*

T A A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*) kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, sasa kwa mujibu wa taratibu zetu za kufanya maamuzi nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Hoja imeshinda, kwa hiyo tutaendelea na utaratibu unaofuata. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU KAMATI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali kwa lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend certain Written Laws*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu tulionao, Muswada huu umekwishamaliza taratibu za Kibunge na kwa hiyo sisi tumeshamaliza kwa nafasi yetu. Kwa mujibu wa Katiba sheria hii sasa itapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili

atoe kibali chake kwa mujibu wa lbara ya 97(1) ili iweze kuwa sheria iliyo kamili.

Nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa aliyoifanya pamoja na watendaji kazi wake wote, Wizara ya Fedha na Mipango na Waziri wao, Waziri wa Fedha na Mipango na Waziri wa Katiba na Sheria na watendaji wenu wote na tunaamini kwamba haya ambayo mmeliomba Bunge hili lirekebishe basi yatakwenda kusaidia ufanisi katika utendaji wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niseme jambo moja kabla Mheshimiwa Spika hajaingia kwa ajili ya kuendelea na utaratibu uliopo mbele yetu. Mheshimiwa Waitara ametumia hoja kwamba marekebisho yake anayaondoa kwa sababu kumekuwa na ubaguzi hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kuna maneno ambayo tukiyasema hapa tuwe tunafahamu hata kamusi inasema nini juu ya maneno hayo, tuwe tunafahamu matumizi ya maneno hayo. Humu Bungeni hakuna mtu yeyote anayebaguliwa na mtu yeyote. Kwa hiyo, hilo lazima lieleweke sawasawa lisije likaenda kwa wananchi kana kwamba kuna Wabunge wengine humu ndani wana hadhi ya tofauti na Wabunge wengine.

Wabunge wote wako sawa kwa mujibu wa Kanuni zetu na kwa mujibu wa sheria zetu na kwa mujibu wa Katiba na ndicho ambacho kinapaswa siku zote kukumbukwa. Ndiyo maana Wabunge wote huwa wanapewa fursa zinazofanana, hakuna Mbunge anayependelewa na hakuna Mbunge yeyote ambaye anaonewa. Kwa hiyo, kauli ikitolewa na Mbunge mwingine ambayo inamuudhi Mbunge mwingine, Kanuni zetu ziko wazi kuhusu nini cha kufanya, tusifike mahali tukaanza kujitolea sisi wenyewe maneno ambayo yatatuma ujumbe ambao si sawasawa kwa wale waliotutuma humu ndani ili tuwawakilishe.

Baada ya kusema hayo, sasa nitampisha Mheshimiwa Spika ili aendelee na utaratibu ulio mbele.

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

SPIKA: Taarifa ya kuahirisha Bunge, Katibu.

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

NDG. DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Saba sasa zimekamilika.

SPIKA: Ahsante sana Katibu kwa taarifa hiyo muhimu, namwona Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko mahali pake. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakukaribishwa kwa ajili ya kutoa hotuba yako. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, leo tumefika mwisho wa Mkutano wa Saba wa Bunge la 11 ulioanza Jumanne ya tarehe nne, mwezi Aprili, mwaka 2017.

Tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuifikia siku hii muhimu, tena baada ya kuwa tumetimiza wajibu wetu wa Kikatiba kikamilifu na kwa umahiri mkubwa. Huu ulikuwa ni mkutano muhimu sana kwa nchi yetu kutokana na jukumu kubwa la kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2017/2018 iliyoanza tangu tarehe 1 Julai, 2017. Bajeti hii ambayo ni nzuri na ya kihistoria ni ya pili tu katika takribani bajeti tano za Serikali ya Awamu ya Tano zitakazoandaliwa hadi kufikia mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako likiendelea tarehe 13 Aprili, 2017 tulipokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Askari Polisi wetu nane

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

waliopoteza maisha wakiwa wanatumikia Taifa kwa kuuawa na kundi la wahalifu katika eneo la Jaribu Mpakani Wilayani Kibiti. Askari hao waliopoteza Maisha ni Mkaguzi Msaidizi Peter Kiguu, *Coplo* Francis, *PC* Haruna, *PC* Jackson, *PC* Zakaria, *PC* Siwale, *PC* Maswi, *PC* Ayoub.

Mheshimiwa Spika, pia hivi karibuni mwezi Juni, 2017, Askari wetu wawili wa kikosi cha usalama barabarani walivamiwa na kupigwa risasi na Majambazi katika Kijiji cha Bungu (B) kilichopo Wilayani Kibiti. Aidha, wananchi wetu wengi wamepoteza maisha kutokana na uhalifu unaofanywa na majambazi waliopo katika maeneo ya Wilaya za Kibiti, Rufiji na Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kulaani kitendo cha kihalifu na kutoa pole kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa kuondokewa na vijana hao shupavu. Aidha, natoa pole kwa familia za wafiwa wote kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mauaji ya wananchi wetu na Askari wetu hayakubaliki na wala hayavumiliki kwani Askari ndiyo Walinzi wetu sisi pamoja na mali zetu. Aidha, tishio kwa walinzi wa amani na wananchi ni tishio kwetu sote hivyo Serikali itahakikisha waliohusika na mauaji hayo wanakamatwa na kuchukuliwa hatua stahiki. Wanaweza kukimbia lakini hawataweza kujificha daima tutawakamata tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asubuhi ya terehe 6 Mei, 2017, nchi yetu iliamka na simanzi kubwa kufuatia ajali iliyogharimu maisha ya watu 36 wakiwemo Wanafunzi 33, Walimu wawili na Dereva mmoja waliokuwa kwenye safari ya kimasomo Wilayani Karatu. Ajali hiyo imezima ndoto za vijana hao na kuacha vilio kwenye familia zao na Taifa zima kwa ujumla. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema roho za marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawaomba Wazazi, Walezi, Walimu na marafiki wa watoto hao waendeleo kumtumainia Mwenyezi Mungu kwa mtihani huo mkubwa walioupata. Naendelea kutoa wito kwa vyombo vyote vinavyohusika na ukaguzi wa vyombo vya moto vya usafiri

kwa wanafunzi na abiria wote, wafanye ukaguzi wa kina na wa mara kwa mara kwenye vyombo vyote vya usafirishaji ili kuliepusha Taifa na ajali zinazozuilika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia ilipata pigo la kuondokea na watumishi wawili wastaafu waliotumikia Taifa hili kwa umahiri mkubwa na uadilifu mkubwa. Watumishi hao ni marehemu Mzee wetu Paul Sozigwa aliyekuwa Katibu wa Rais wa Awamu ya Kwanza na marehemu Said Mwambungu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Namwomba Mwenyezi Mungu awape pumziko la amani Marehemu wote baada ya kutumikia Taifa letu kwa utumishi uliotukuka na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge; katika Mkutano huu Bunge lako Tukufu limejadili na kupitisha bajeti za Wizara zote 19 na bajeti nzima ya Serikali Kuu. Kupitisha maazimio matano ya kuridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kupitisha Miswada ya Sheria mbalimbali ambayo ni Muswada wa Sheria ya Fedha za matumizi; Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017; Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi wa mwaka 2017 na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali 499 ya msingi na mengine 1,834 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri na maswali ya papo kwa papo pia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yaliulizwa. Katika kipindi hiki, Ofisi ya Bunge iliendesha semina mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi na kuwapa uelewa mpana wa masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lilipata fursa ya kuchagua Wawakilishi wa Tanzania kwenye Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Wabunge tisa walichaguliwa; kati ya Wabunge hao, Wabunge watano ni

Wanawake na Wabunge wanne ni Wanaume. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge hao wataiwakilisha nchi yetu vyema na kwamba watatimiza kikamilifu wajibu wao kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki inaelekezwa kufanya kazi kwa karibu na Wabunge hao ili kuwasaidia kwa namna moja au nyingine na kuwapa ushirikiano unaostahili ili waweze kutekeleza vizuri majukumu yao kwenye Bunge hilo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yake, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Watendaji, Wataalam wa Serikali katika vitengo mbalimbali pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha kazi zote zilizopangwa kwenye Mkutano huu tena kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa maelezo mazuri na ufafanuzi waliutoa katika kujibu maswali mengi ya msingi na ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na kujibu hoja za Kamati za Kudumu za Bunge na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge binafsi ndani ya Bunge zima. Serikali inathamini sana maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge mliotoa kwa Serikali na tunaahidi kuendelea kuzingatia maoni yenu na ushauri wenu na tunawaahidi kwamba pale ambako tumeshauriwa tutaweza kutekeleza ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais; tarehe 14 Juni, 2017 Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua anazochukua kukabiliana na upotevu wa mapato ya Serikali katika Sekta ya Madini. Aidha, tarehe 29 Juni, 2017 Bunge lako lilikubali kwa kauli moja ya kuridhia mabadiliko ya ratiba ya Mkutano huu wa Bunge la bajeti ili kuongeza siku 5 za kazi kwa lengo la kuwezesha kujadili

Miswada mitatu ya mwaka 2017 inayohusu kulinda maslahi na rasilimali za Taifa ikiwemo madini. Hii inadhihirisha kwamba Bunge hili ni la wananchi na linazingatia maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri, juhudi na hatua stahiki anazoendelea kuchukua ili kuhakikisha kwamba Watanzania na Taifa kwa ujumla wananufaika na rasilimali za Taifa. Nawasihi wananchi wote na viongozi tuendeleo kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu katika jitihada zake hizo na kulinda maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama; kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama nchini ni shwari, usalama wa raia na mali zao unaendelea kulindwa na mipaka yote ya nchi yetu iko salama. Aidha, vikosi vya ulinzi na usalama viko imara na madhubuti katika kulinda mipaka na usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, wapo baadhi ya wenzetu wanaotishia usalama wetu kwa kushiriki kwenye vitendo vya uhalifu kwa kutumia silaha. Mathalani, katika miezi ya hivi karibuni, kumekuwa na mauaji ambayo nimeyaeleza awali ya kuvizia katika maeneo ya Mkuranga, Kibiti na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kila raia wa Tanzania wakiwemo Wananchi wa Wilaya hizo za Mkuranga, Kibiti na Rufiji wanakuwa huru kufanya shughuli zao za maendeleo bila kuhofia usalama wa maisha yao. Serikali inaendelea kuchukua hatua za muda mfupi na za muda mrefu ili kuerejesha hali ya usalama katika maeneo hayo. Tumeongeza doria na vitendea kazi kwa Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumefanya maamuzi ya kuunda Kanda maalum ya Kipolisi katika Mkoa wa Pwani itakayojumuisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji na tayari Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo maalum amekwishateuliwa. Hivyo, natoa wito kwa raia wema katika Wilaya hizo waendeleo kutoa ushirikiano kwa Serikali ili kuwezesha watuhumiwa wote kukamatwa.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sanjari na mikakati ya kudhibiti uhaifu unaofanywa ndani ya nchi, tunaendelea pia kudhibiti uhalifu unaovuka mipaka (*cross boarder crimes*) ili kutimiza jukumu hilo. Tunaendelea kuboresha huduma za uhamiaji na kudhibiti nyaraka zinazotolewa na idara ya uhamiaji, tumeanzisha mfumo wa kuhakiki nyaraka hususani vibali vya kuishi nchini pamoja na hati za kusafiria. Vile vile tumehuisa utaratibu wa Kisheria wa kutoa *migrant pass* kwa Wahamiaji walowezi ili kuweza kuwatambua kwa urahisi zaidi. Kwa jitihada hizi, tutaweza kudhibiti nyaraka za kughushi na kudhibiti uhalifu wa Kimataifa unaovuka mipaka.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa maafa; katika msimu wa masika, baadhi ya maeneo ya nchi yetu yalipata mvua za juu ya wastani na hivyo kusababisha maafa na madhara kwa wananchi ikiwemo vifo, majeruhi na uharibifu mkubwa wa makazi na miundombinu mbalimbali. Mikoa iliyoathirika zaidi ni pamoja na Kagera, Tanga, Arusha, Dar es salaam na visiwa vya Unguja na Pemba. Kutokana na mvua hizo, watu 15 walipoteza maisha, watu 78 walijeruhiwa, nyumba 1,845 na majengo 36 ya Taasisi mbalimbali yaliharibiwa katika viwango tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile miundombinu ya barabara 48 katika mikoa 11 iliathiriwa na hivyo kuzorotesha kwa muda usafiri na usafirishaji katika maeneo husika. Aidha, viwanja vya ndege vya Arusha, Musoma, Ziwa Manyara, Mafia na Sumbawanga navyo viliathirika na mvua hizo. Natoa pole kwa waathirika wote kwa kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliiana na athari za mvua hizi, Serikali iligharamia matibabu ya majeruhi na mazishi kwa waliopoteza maisha. Aidha, Serikali imetoa misaada ya kibinadamu kama vile chakula, dawa, nguo na kufanya matengenezo ya dharura kwa miundombinu iliyoharibika. Zoezi la ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua liliendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na kutoa elimu kwa umma kuhusu menejimenti ya maafa hususani kuzuia,

kukwepa na kuweka mipango thabiti kwa wananchi kujiandaa na maafa ili kupunguza athari za maafa pindi yanapotokea. Aidha, tutaendelea kutoa taarifa za utabiri wa hali ya hewa mara kwa mara na kwa wakati ili kutoa fursa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wananchi kujiandaa vyema. Tutakamilisha mifumo ya ufuatiliaji wa maafa kwenye Kituo chetu cha Uratibu wa Mawasiliano Wakati wa Dharura, kuainisha na kutambua maeneo hatarishi kwa maafa pamoja na kuendelea kujengea uwezo idara yetu ya uratibu wa maafa.

Mheshimiwa Spika, naomba niizungumzie Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018. Nikiwa natambua kwamba, Bunge lako limejadili kwa kina mipango yote hii, hapa nitakachokifanya ni kueleza kwa kifupi yale yaliyojitokeza. Kuanzia tarehe 4 Aprili, 2017 hadi tarehe 20 Juni 2017 Bunge lako Tukufu lilipokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara na Taasisi mbalimbali hapa nchini na hasa za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama. Aidha, Bunge lilipokea na kujadili hoja ya Serikali kuhusu hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016, Mpango wa Maendeleo pamoja na makadirio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 ya jumla ya shilingi trilioni 31.7.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dokta Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake Mheshimiwa Dokta Ashatu Kijaji kwa hotuba nzuri ya mpango wa maendeleo ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018. Nawapongeza pia Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa umakini mkubwa, kwa maandalizi ya bajeti yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuhitimisha hoja hiyo. Kipekee kabisa, nawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hoja za maboresho na kwa kupitisha bajeti ya Serikali kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kura za Waheshimiwa Wabunge kupitisha bajeti ya mwaka 2017/2018 ni kielelezo kwamba Bajeti hii inajibu kiu ya wananchi ambayo ninyi Waheshimiwa Wabunge mnawakilisha kupitia michango yenu na kwa pongezi zenu kwa Serikali. Nimepata faraja kwamba mnathamini na kuheshimu usikivu wa Serikali yetu kwa maoni ya wananchi ambao mmekuja kuwawakilisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ni sikivu, Serikali hii ni makini na Serikali hii inazingatia maslahi ya wananchi walio wengi na hasa wa kipato cha chini. Hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali siyo tu itaendelea kusikia bali itasikiliza na kuchukua hatua kama tulivyofanya kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa kufuta kodi mbalimbali za kero hasa katika kilimo na mifugo ili kuwawezesha wananchi kuongeza kipato kwa kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako kuidhinisha bajeti ya Serikali, tutahakikisha tunasimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2017/2018. Tayari tumeandaa mkakati wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo ambao unaainisha hatua za utekelezaji, vigezo vya kupima ufanisi na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa katika kukamilisha miradi husika. Vilevile tunaandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miradi ya maendeleo (*National project data Bank*) ili kufuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa miradi na changamoto zinazokabili kwa lengo la kuikwamua.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hatua hizo, Serikali imetoa maelekezo kwamba; vitengo vya ufuatiliaji na tathmini viimarishwe na kupewa nyenzo stahili ili vifuatilie miradi ya maendeleo hatua kwa hatua. Shabaha yetu ni kuhakikisha kuwa, miradi inasimamiwa kikamilifu, inaleta tija na kutekelezwa kwa ubora na viwango vilivyoainishwa kwenye mikataba iliyofungwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, mipango tuliyojiwekea haiwezi kufanikiwa endapo tutazembea katika kukusanya kodi na mapato ya Serikali;

hivyo Serikali itaendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato, kuimarisha ukusanyaji wa mapato yenyewe, kudhibiti biashara za magendo, kuhimiza matumizi ya mashine za kielektroniki katika kukusanya mapato na kudhibiti udanganyifu katika ukadiraji wa ushuru wa forodha. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kuhakikisha kuwa, tunashirikiana na Halmashauri tunakotoka kubuni vyanzo vya mapato na kuhamasisha ulipaji wa kodi bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, kulipa kodi ni uzalendo na tuhamasishe wananchi wenzetu waone fahari kuwa sehemu ya mafanikio ya nchi yetu kwa kulipa kodi na kuwafichua wakwepa kodi. Ahadi yetu ni kuendelea kuisimamia kila senti itakayokusanywa ili itekeleze jukumu lililokusudiwa. Aidha, tutaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ili kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa zinatumiwa kwa umakini na kuleta tija kwa maendeleo ya nchi yetu. Tulipe kodi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo; hali ya chakula nchini; napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hali ya chakula siyo ya kuridhisha sana, bado kuna maeneo yenye upungufu wa chakula. Pia yapo maeneo yaliyopata mvua nyingi ambayo yamepata chakula cha kutosha. Hii ni kutokana na mazao ya chakula katika maeneo hayo kuanza kukomaa. Aidha, kutokana na wakulima katika baadhi ya maeneo kuanza kuvuna mazao yao, mwenendo wa bei za vyakula hususani mahindi imeanza kushuka katika masoko mbalimbali. Hata hivyo, kutokana na nchi zinazotuzunguka kuwa na upungufu mkubwa wa chakula na umuhimu wa kuwa na usalama wa chakula na kujitosheleza kwa hifadhi ya chakula, ni vizuri kila Kaya ikahakikisha kwamba inakuwa na akiba ya chakula kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, aidha, tumepiga marufuku usafirishaji wa mahindi nje ya nchi bila kibali. Narudia tena; tumepiga marufuku usafirishaji wa mahindi nje ya nchi bila kibali badala yake tunahamasisha uongezaji wa thamani ya

mazao hayo badala kusafirisha nafaka ghafi. Hii inatokana na kuwepo na maeneo ambayo hadi sasa hayana chakula cha kutosha. Nawashauri wafanyabiashara wa ndani wasambaze mahindi huko ambako kuna upungufu mkubwa. Aidha, natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa ya mipakani kutekeleza agizo la Serikali la kuchukua hatua kali kwa wanaokiuka agizo la kutoa chakula ghafi nje.

Mheshimiwa Spika, mfumo mpya wa usambazaji wa mbolea; Serikali inajipanga vyema msimu ujao wa kilimo kwa kusambaza pembejeo na kuhamasisha matumizi ya mbolea. Ili kufanikisha azma hiyo, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali imeamua kuimarisha utaratibu wa upatikanaji na usambazaji wa mbolea kupitia mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja (*fertilizer bulk procurement system*).

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo huo, mbolea itaagizwa na Waagizaji watakaopitishwa kwenye utaratibu wa zabuni za wakulima wataoweza kununua mbolea hiyo katika maduka ya pembejeo vijijini kwa bei dira itakayopangwa na Serikali. Mfumo huo mpya utanza kwa kuingiza mbolea ya kupandia aina ya *DAP* na mbolea ya kukuzia aina ya *UREA* ambazo zinatumiwa na wakulima wengi. Mbolea za aina nyingine zitaendelea kuletwa kwa utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea maelekezo yangu kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwamba isimamie kikamilifu zoezi hili la usambazaji wa mbolea na ili kuhakikisha kwamba mbolea inawafikia wakulima miezi miwili au mitatu kabla ya msimu wa kilimo haujaanza.

Mheshimiwa Spika, Maboresho kwenye Sekta ya Mifugo; pamoja na idadi kubwa ya mifugo tuliyonayo nchini, lakini mchango wake kwenye pato la Taifa katika kutuingizia fedha za kigeni sio wa kuridhisha. Kutokana na hali hiyo tarehe 15 Juni, 2017, nilikutana na Maafisa Mifugo wa Wilaya zote nchini kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja ya kuboresha sekta ya mifugo nchini ili iweze kuleta tija na kuongoza mchango wake kwenye pato la Taifa.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mikakati tuliyojiwekea, ni pamoja na kuwawezesha wafugaji kupata maeneo mahususi ya malisho ya mifugo yao na kuwapatia mafunzo ya ustadi wa ufugaji bora. Vile vile tumetoa maelekezo kwa Maafisa Mifugo kuwatembelea wafugaji ili kuwahudumia na kuwapa mafunzo ya ufuaji bora. Aidha, tumezindua mwongozo wa ufugaji bora nchini, ambao utakuwa ni dira ya kuwaongoza wafugaji kuhusu namna ya kuboresha sekta ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuwa na mifugo michache lakini yenye tija kubwa. Hata hivyo, tumekemea wafugaji wasilishe mifugo yao kwenye mashamba yenye mazao ya chakula na pia kuchungia kwenye misitu iliyohifadhiwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaokiuka agizo hilo au katazo hilo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ardhi; Upimaji na Umiliki wa Ardhi, ardhi isiyopimwa ina thamani ndogo na ni chanzo cha migogoro isiyokuwa ya lazima. Chama cha Mapinduzi iliona jambo hili na kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015, ilielekeza Serikali kuhakikisha kuwa kila kipande cha Ardhi ya Tanzania kinapimwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeweka mkakati wa Mpango Kazi wa kuwazesha kufikia lengo la kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji 1500 na Wilaya tano kila mwaka. Aidha, Serikali inaendelea kuchukua hatua stahiki za kupunguza gharama za umilikaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali imepunguza tozo ya mbele (*Premium*) kutoka asilimia 7.5 ya thamani ya ardhi hadi asilimia 2.5 tu. Natoa wito kwa wananchi kuchangamkia punguzo hili na kujitokeza kwa wingi kupimiwa ardhi ili waweze kumilikishwa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha huduma za Ofisi ya Ardhi za Kanda; kazi ya upimaji wa ardhi haiwezi kufanikiwa bila rasilimali watu. Serikali itaendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi

za Kanda kwa kupeleka wataalam wa kada mbalimbali za kuwawezesha kwa kuwapatia vitendea kazi stahiki. Lengo letu ni kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za ardhi katika kanda, badala ya kufuata huduma hizo Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nawasihi watumishi watakaohamishiwa katika Ofisi za Kanda pamoja na wale waliopo katika halmashauri, wafanye kazi kwa ushirikiano na watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Ardhi. Nakutoa huduma kwa wananchi bila ya ubaguzi, bila ya usumbufu na bila ya kuomba rushwa ya aina yoyote ile. (*Makofi*)

Sekta ya Wanyamapori; Hifadhi ya mapori, asilimia 28 ya eneo la nchi yetu limetengwa kwa ajili ya kuhifadhi rasilimali za Taifa zikiwemo misitu, wanyamapori na utunzaji mazingira kwa ajili ya matumizi ya binadamu na viumbe hai, wakiwemo wanyamapori ambao wanachangia kwa kiwango kikubwa katika shughuli za utalii. Changamoto kubwa iliyopo sasa katika mapori yetu ya hifadhi ni uvamizi wa mifugo na kwa bahati mbaya sana kwenye Mikoa ya Mipakani mifugo mingi imekuwa ikitoka nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Hifadhi za Taifa na Mbuga zetu za Wanyamapori zinalindwa kikamilifu, mwezi Novemba, 2016, niliigiza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, kuweka alama za mipaka (*beacons*), kuainisha maeneo yote ya hifadhi nchini kwa lengo la kuondoa migogoro iliyopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuweka alama hizo Serikali imeanza rasmi zoezi la kuondoa mifugo yote ndani ya hifadhi. Aidha, nimeelekeza kwamba uwekaji wa alama au nguzo hizo uhusishe Halmashauri za Wilaya na Ofisi za Wakuu wa Wilaya ili kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima. Ramani zinazoonesha mapori zitumike kubainisha wazi katika uwekaji wa alama hizo. Aidha, mapori yote yaliyohifadhiwa kisheria yaendelee kuheshimika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwepo kwa migogoro baina ya wafugaji na wakulima na migogoro baina ya wafugaji na wahifadhi wanyamapori, nimeelekeza kwamba ifikapo mwisho wa mwezi Julai, 2017, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wabainishe ma eneo yote ya *ranch* za Taifa za Mifugo, ambazo hazitumiki na kuzigawa katika vitalu *blocks* kwa wafugaji ili mifugo mingi iondolewe vijijini na ipelekwe kwenye maeneo hayo ili Serikali iweze kutoa huduma za ugani za kisasa huko kwenye hizo *blocks*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wafugaji wote nchini kufuata Sheria za Hifadhi za Taifa, Mbuga za Wanyamapori, Maeneo Tengefu pamoja na Vyanzo vya Maji. Mifugo yote itakayokutwa ndani ya hifadhi, maeneo yote hayo ambayo nimeyataja hatua kali zitachukuliwa na kufikishwa Mahakamani. Aidha, tukumbuke kuwa ardhi haiongezeki, lakini wafugaji na mifugo vinaongezeka. Hivyo, ni lazima tufuge kisasa na tufuge mifugo michache yenye tija, ambayo tutaweza kuihudumia katika maeneo tuliyonayo na ambayo tumeyatenga kwa ajili ya ufugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya; Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba; kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza kuhusu umuhimu wa afya bora kwa wananchi wetu, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha upatikanaji wa dawa za vifaa tiba, kwa kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa tiba pamoja na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 236 zikiwa ni fedha za ndani kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali imetenga fedha za ndani tena, kiasi cha shilingi bilioni 33 kwa ajili ya chanjo za watoto na makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wazazi, walezi, kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata chanjo zote zinazotakiwa ili kuwakinga na magonjwa na kuwajengea misingi mizuri kwa maisha yao ya baadaye. Aidha, kila mwananchi ajenge utamaduni na utaratibu wa kupima afya yake mapema ili kubaini tatizo lake la kiafya, baada ya kusubiri hadi ugonjwa ufikie hatua mbaya ndipo aende

hospitalini. Katika hatua hii ya Serikali yetu ya kuboresha huduma za afya, hakuna sababu ya mwananchi kubaki akiwa hajui afya yake.

Mheshimiwa Spika, Vifo vitokanavyo Uzazi; tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto kubwa katika nchi yetu. Takwimu za hivi karibu zinaonesha kuwa idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Hali hii haikubaliki na haivumiliki, kwani wanaopoteza maisha ni Watanzania wenzetu, ni mama zetu na ni wake zetu, ni dada zetu na ni watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia maoni na michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili wakati wote mkiwa hapa Bungeni kwenye mijadala yetu ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bajeti ya Wizara ya Afya, Bajeti ya Serikali Kuu iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imewasikia na kwa hakika inaguswa sana na vifo vitokanavyo na uzazi, ndio maana Serikali imeamua kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha Huduma za Afya ya Mama na Mtoto, Mama na Uzazi. Serikali imeamua kwamba, itanunua kusambaza na kutoa bila malipo dawa kwa ajili ya uzazi salama katika vituo vya umma vya kutolea huduma. Hii ni pamoja na da wa za kuzuia kutokwa na damu baada ya kujifungua, dawa kwa ajili ya kifafa cha mimba, dawa kwa ajili ya kuongeza damu. Jumla shilingi bilioni saba zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imejizatiti kuongeza kasi ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati vijijini pamoja na kuimarisha vituo vyote vya kutolea tiba nchini kwa lengo la kuboresha huduma za afya. Hivyo, napenda kuwahakikishia akinamama wote nchini kwamba hakuna mwanamke mjamzito atakayepoteza maisha kwa kukosa dawa, sindano ya kuzuia kuvuja damu au kukosa dawa za kuzuia kifafa cha mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa watoa huduma kwenye maeneo yetu ya kutolea huduma; Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Rufaa za Mikoa kuhakikisha kwamba akinamama wanapokelewa vizuri, wanatibiwa vizuri ili kuwaondolea adha na kuwaondoa kwenye dimbwi la vifo ambavyo si muhimu na kila mmoja awajibike kwa nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu; Kuinua Ubora wa Elimu na Mafunzo; kwenye hotuba yangu ya kufungua Mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu unaoahirishwa leo hii, nilieleza kwa kirefu umuhimu wa watoto wetu kutoa kipaumbele kwa masomo ya sayansi. Nilisema endapo watoto wetu hawatasoma masomo ya Sayansi, watabaki kuwa watazamaji kwenye Uchumiwa Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeanza kutimiza wajibu katika kuweka mazingira wezeshi kwa watoto wetu kujifunza masomo ya Sayansi kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 6 Juni, 2017 nilizindua zoezi la usambazaji wa vifaa vya maabara kwa ajili ya shule ya sekondari 1696, vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.9. Vifaa hivyo vitaendelea kusambazwa katika shule za Tanzania Bara ambazo zimekamilisha ujenzi wa maabara. Hivyo, natoa wito kwa wanafunzi kutumia vifaa hivyo kusoma kwa bidii masomo ya sayansi na kuvitunza ili vinufaishe wanafunzi wengi zaidi. Aidha, Halmashauri zote nchini ambazo hazijakamilisha ujenzi wa maabara, zinaelekezwa kukamilisha zoezi hilo mapema ili vifaa vingine vitakapoletwa visambazwe haraka kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Elimu Jumuishi; sanjari na jitihada za kuinua ubora wa elimu nchini, Serikali imeendelea kutafuta suluhu ya changamoto za kujifunzia zinazowakabili wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hivi karibuni Serikali imenunua vifaa kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wenye baki ya usikivu na kuvisambaza katika shule 213 za msingi na shule 22 za sekondari.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imenunua vifaa vya upimaji ili kubaini watoto wenye mahitaji maalum ya ujifunzaji kwa Mikoa yote Tanzania Bara. Rai yangu kwa wazazi wenzangu kote nchini, ni kutumia fursa hii kuwapeleka shuleni watoto wenye mahitaji maalum badala ya kuwaficha majumbani. Shabaha ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Tanzania mwenye umri wa kwenda shule anapata fursa hiyo bila kujali uwezo wake wa kifedha au changamoto za kimwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msimamo wa Serikali kuhusu Ujauzito Shuleni; moja kati ya mijadala iliyoibua hisia kali wakati wa mjadala wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni pamoja na kuwaachisha watoto masomo wanafunzi waliopata ujauzito shuleni. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015, jumla ya wanafunzi 3,637 waliacha masomo kutokana na kupata ujauzito. Kuwaachisha masomo wanafunzi waliopata ujauzito ni utekelezaji wa waraka na kanuni ya mwaka 2002 zinazohusu kufukuza na kuondoa wanafunzi shuleni kutokana na makosa mbalimbali ikiwemo uasherati, wizi, ulevi, kutumia dawa za kulevya pamoja na utoro unaotokana na baadhi ya wanafunzi kwenda kufanya shughuli za biashara ndogo ndogo, kucheza kamali, kuvua samaki, kuchimba madini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali wa kutoruhusu wanafunzi waliopata ujauzito kuendelea na masomo katika mfumo rasmi wa elimu ni kwa mujibu wa sheria na wala sio utaratibu mpya kama inavyopotoshwa na baadhi ya wanaharakati. Msimamo huo wa kisheria unalenga kuwafanya watoto wa kike wajishughulisha na masomo yao badala ya kushiriki kwenye vitendo vya ukiukwaji wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, lengo hili pia nalo ni kuwaelimisha wazazi, kila mzazi aendelee kumtunza na kumwelimisha mtoto wake mambo muhimu na maadili mema ndani ya familia. Wazazi wajishughulisha kikamilifu katika kuweka katazo kwa watoto kujishirikisha na ngono wakiwa na umri mdogo. Dhamira ya Serikali katika hili, ni

kumlinda mtoto wa kike ili apate elimu kwa ajili ya manufaa yake ya Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tutakumbuka Kauli Mbiu ya Mke wa Rais wa Awamu ya Nne Mama Salma Rashid Kikwete aliyesema "*Mtoto wa Mwenzi ni Mwanao.*" Ni budi kila mzazi akajikita katika kuwalea watoto hawa badala ya kuwafanyisha vitendo ambavyo havistahili, kwa kauli ile ile kwamba mtoto wa mwenzi ni wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania ana wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu. Hivyo ni lazima tihakikishe mtoto wa kike anapata elimu stahiki na masomo yake hayakatizwi kwa kupata ujauzito. Kama ambavyo nimeendelea kurudia, kuwa Serikali imewekeza kwa elimu ya mtoto wa kike nchini. Kwa hiyo ni budi kila mmoja akazingatia uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu Namba 60(b) cha Sheria ya Elimu Sura ya 353 kinatoa adhabu ya miaka 30 jela kwa yoyote atakayeoa au kumpa ujauzito mwanafunzi. Aidha, sheria inatoa adhabu ya kifungo cha miaka mitano jela au faini ya shilingi milioni tano au vyote kwa pamoja kwa anayeshiriki kumwozoshwa mtoto wa shule. Natoa wito kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, pamoja Maafisa Elimu kusimamia utekelezaji wa sheria ya nchi yenye lengo la kumlinda mtoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tushirikiane na halmashauri zetu kuweka mikakati ya kudhibiti ujauzito kwa wototo wetu. Wakati wote tutoe karipio kwa wale ambao wanajihusisha na kuharibu mwenendo wa watoto wetu, wahamasisheni wananchi watoe ushirikiano kwa vyombo vya dola ili wanaowapa wanafunzi ujauzito au kuwakatiza masomo au kuwaozesha wapate adhabu kali inayostahili kwa matendo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; katika mjadala wa bajeti, moja kati ya sekta ambayo Waheshimiwa Wabunge

wengi wallionesha kwamba inahitaji kupewa kipaumbele cha pekee ni Sekta ya Maji. Hakika nami nakubaliana na mtazamo huu wa Waheshimiwa Wabunge kwani maji ni uhai na kichocheo cha Maendeleo katika sekta mbalimbali na nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya umaskini. Serikali nayo pia inakubaliana na hili kuwa upo muhimu sasa wa kuongeza nguvu kwenye sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la maji lilitolewa ufafanuzi wa kina na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, naomba Waheshimiwa Wabunge watuelewe kwamba tumewasilikiliza na tumewasikia. Serikali inayo nia ya dhati kuhakikisha kwamba vijiji vyetu zaidi vinapata huduma ya maji.

Mheshimwia Spika, Uboreshaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa Nchini; Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini zinatimiza malengo ya kuanzisha kwake na kwa mujibu wa ibara ya 143 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuendeleza juhudi za ugatuaji wa madaraka kwenda katika vyombo hivyo, pamoja na kuongeza mgao wa fedha za ruzuku ya maendeleo inayopelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018, imetenga kiasi cha shilingi bilioni 412.38 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 16.985 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya majengo ya ofisi na makazi ya viongozi katika mikoa yote mipya. Katika mgao huo, Mkoa wa Njombe umetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.34; Mkoa wa Katavi umetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.080; Mkoa wa Simiyu umetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.775; Mkoa wa Geita umetengewa shilingi bilioni 2.978; na Mkoa wa Songwe umetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.812.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 61.7 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri 64, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 28.7 ni kwa ajili ya kukamilisha majengo ya Ofisi katika Halmashauri 44 na shilingi bilioni 33 ni kwa ajili ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri mpya 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala mpaka tukamilishe maeneo ambayo tumeyateua kwa kuongeza miundombinu. Sambamba na hatua hizo, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto imetoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye thamani ya shilingi bilioni 2.9, pamoja na kununua magari ya kubebea wagonjwa katika halmashauri 67.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea na mpango mahususi wa kuwajengea uwezo Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji pamoja na Watendaji wa Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji ili waweze kutoa huduma bora nakwa ufanisi katika kuwahudumia wananchi. Sehemu ya fedha za maendeleo zitatumika kwa ajili ya kujenga uwezo wa watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali za kuimarisha utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na kutatua kero zao katika ngazi hiyo. Aidha, jitihada hizo zimeleza kuongeza kasi ya maendeleo vijijini na kuboresha maisha na ustawi wa wananchi wetu. Kwa msingi huo, natoa wito kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya, pamoja na Halmashauri zetu zote nchini, wahakikishe kwamba malalamiko yote ya wananchi yanatatuliwa haraka katika ngazi husika. Si vyema na haikubaliki kwa wananchi kusafiri umbali mrefu kwa mail nyingi kutafuta suluhu za changamoto zao kwa viongozi wa kitaifa, wakati mamlaka za Serikali za Mitaa zipo na zina viongozi wanaolipwa mishahara na kwa fedha za walipa kodi. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa watumishi wote walioko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuhakikisha kuwa wanatembelea vijiji, wanaitisha mikutano vijijini na kuzungumza na wananchi kwa lengo la kusikiliza kero na kutoa ufumbuzi wa kero zao. Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo haya ninayotoa leo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na kero zao pale mahali walipo.

Mheshimiwa Spika, Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya; Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya uzalishaji, uuzaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya nchini. Tumeendelea kubaini mtandao wa waingizaji wa dawa hizo hapa nchini na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahalifu hao. Ili kuimarisha mapambano hayo na kuyaendesha kisayansi, Serikali imekamilisha uteuzi wa watendaji mahiri wa Mamlaka za Kupambana na Dawa za Kulevya, wanaojumuisha Makamishna wanne waliobobea kwenye taaluma zao na wenye uzoefu na uzalendo mkubwa kwenye mapambano haya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi cha kuanzia mwezi Februari mwaka huu wa 2017 mamlaka hii ilipozinduliwa imefanikiwa kukamata watuhumiwa 4,809 wakiwa na dawa za kulevya aina ya *Heroin*; gram 327.173; *Cocain*, kilo 26,977; bangi, kilo 18,334.83; mirungi, kilo 11,306.67; na lita 6,338 za kemikali bashirifu zilizokamatwa bandarini ambazo hutumika kutengeneza madawa kama *Heroin* na *Cocaine*. Aidha, mamlaka kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zimeendelea kufanya *operation* ya kuteketeza ekari 569.25 za mashamba ya bangi na hekari 64.5 za mashamba ya mirungi na kazi hiyo inaendelea. Kutokana na hatua hizo jumla ya majalada ya kesi 3,222 yamefunguliwa hizo ndio jitihada za mamlaka yetu.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya zina athari kubwa kwa ustawi wa familia zetu na Taifa kwa ujumla hivyo napenda kurejea wito wangu kwa Watanzania wote kuunga mkono jitihada za Serikali katika mapambano haya kwa

kuendelea kutoa taarifa kuhusu watu wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Aidha, naendelea kutoa rai kwa wazazi wenzangu kufuatilia mienendo ya watoto wetu ili wasijiunge katika makundi mabaya ya kujihusisha na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba waathirika wa kubwa wa dawa za kulevya ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 35 kundi ambalo ni tegemeo kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kutokomeza kabisa mtandao wa dawa za kulevya nchini kwa kuhakikisha kuwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanakuwa endelevu. Yanafanyika kisayansi na yataleta mafanikio makubwa tuungeni mkono kwenye mapambano haya ili tutokomeze kabisa mtandao huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Michezo; wakati vikao vya Bunge hapa vikiendelea timu yetu ya vijana walio chini ya umri wa miaka 17, Serengeti *Boys* ilishiriki na kutoa upinzani mkubwa sana kwenye mashindano ya shirikisho la mpira wa miguu Barani Afrika ambapo ilimaliza ikiwa na jumla ya *point* nne sawa na timu iliyoshika nafasi ya pili. Hata hivyo, kutokana na Kanuni tu za mashindano hayo Serengeti *Boys* haikuweza kuendelea na mashindano pamoja na matokeo hayo mazuri.

Mheshimiwa Spika, binafsi nilifuatilia sana mechi zote za Serengeti *Boys*, nikiri kwamba vijana hawa wana vipaji na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yao. Kwangu mimi vijana wale ni washindi bila hata wangukuwa wamepewa taji lolote. Naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwapongeza sana kwa dhati kudhihirisha kwamba hakuna linaloshindikana tukiamua. Msisitizo wangu kwa *TFF*, shirikisho la soka Tanzania ni kuendelea kuwatunza vijana hao na kusimamia vilabu vya michezo nchini, kuwekeza kwenye soka la vijana ili tujenge timu imara kwa miaka michache ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa michezo kwa afya, umoja wa kitaifa na kama fursa ya ajira kwa vijana wetu. Wiki iliyopita Mkoani Mwanza yamehitimishwa mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA, wananchi wa Mwanza na Watanzania kwa ujumla wamejionea uwezo wa michezo wa vijana wetu, vipaji na hamasa kubwa iliyoko miongoni mwa vijana wetu kutumia vipaji vyao, hivyo, tutaendelea kuratibu michezo mashuleni kote nchini, ikiwa ni pamoja na kusimamia ufundishaji wa michezo shuleni kama somo.

Mheshimiwa Spika, maelekezo yetu ni kwamba kila mkoa uwe na shule angalau mbili zenye mchepuo wa michezo na Walimu wenye sifa stahiki za kufundisha michezo. Nawapongeza sana Walimu wetu kwa kusimamia vizuri michezo shuleni, nitumie fursa hii kuwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini wahakikishe kwamba kila shule inakuwa na viwanja vya michezo mbalimbali na wanapata nafasi ya kucheza michezo mbalimbali na Walimu wapate nafasi ya kusimamia michezo hiyo ili kuwapa fursa wanafunzi kushiriki michezo ili kupandisha na kuinua vipaji vyao na Walimu wanahimizwa wasimamie michezo hiyo shuleni kila mmoja kwa fani yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadhamini walliodhamini michezo yetu ya UMITASHUMTA na UMISETA kule Mkoani Mwanza mwaka huu 2017. Ambao ni *Coca Cola Kwanza Company* iliyoweza kutoa mchango mkubwa sana, *LAPF* imeweza kutoa mchango wake, Chama cha Walimu Tanzania nacho pia kimeweza kutoa mchango mkubwa na wale wote ambao wametoa michango yao tunawashukuru sana na tunaendelea kuwategemea kuwa mtaendelea kutuunga mkono ili kuendeleza kiwango cha michezo nchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kitendo chake cha kuunga mkono jitihada za michezo nchini kwa dhamira yake ya kujenga uwanja mkubwa wa michezo hapa Mjini Dodoma,

Makao Makuu ya nchi, kwa kushawishi mataifa rafiki kama vile Morroco ambao wameamua kutujengea uwanja mkubwa sana wa michezo hapa makao makuu ya nchi Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kusimamia michezo nchini na Serikali hii haitafumbia macho usimamizi mbovu na utawala wa mchezo usiojali maslahi ya Taifa. Serikali imeazimia kuzimia kusimamia kuimarisha utendaji wa vyombo vya michezo nchini ili kila mwenye dhamana awajibike ipasavyo. Kwa msingi huo, leo hii naelekeza kwa Waziri mwenye dhamana ya michezo nchini kulifanyia mapitio na kutathimini upya Baraza la Michezo Tanzania ili kujiridhisha na usimamizi wake wa shughuli za michezo nchini. Pale itakaporidhika kwamba usimamizi bado sio imara, anayo ruhusa ya kulivunja na kuunda Baraza jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nirejee masuala makubwa yaliyosisitizwa wakati nafungua Mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu. Masuala hayo niliyoyasisitiza ambayo naamini bado yana umuhimu hadi sasa kwa ustawi wa nchi yetu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Tuendeleo kulinda na kudumisha amani nchini ili wananchi washiriki shughuli za maendeleo bila hofu ya usalama wao. *(Makofi)*
- (ii) Jukumu la kujenga uchumi wa nchi yetu ni wajibu wa kila mwananchi na ni lazima kila mwananchi afanye kazi kwa bidii na maarifa ili apate stahiki na afichue wanaokwepa kulipa kodi.
- (iii) Tujenge utamaduni wa kupima afya zetu na kufanya mazoezi ya viungo ili kujilinda na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanaigharimu sana nchi yetu kwa kudhoofisha miili yetu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- (iv) Tuepuke matumizi mabaya rasilimali zetu kama vile maji, madini na msitu ili zinufaishe kizazi chetu na vizazi vijavyo.
- (v) Tuzingatie matumizi ya muda, tuongeze nidhamu na uwajibikaji, tuzingatie muda wa kupiga vita tamaduni zote zinazohamasisha uvivu na uzembe.
- (vi) Pia mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuwa ni janga kubwa linaloitafuna nchi kwa kasi kubwa na kupoteza nguvu kazi ya nchi yetu. Tunahitaji ushiriki wa kila mmoja katika vita hii kwa kufichua mtandao wa wahusika wa dawa za kulevya.
- (vii) Hamasa kwa michezo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnashiriki kwenye michezo mbalimbali tunatoa wito kwa Watanzania wote kushiriki kwenye michezo mbalimbali ikiwemo na *jogging* pamoja na mazoezi ya viungo mbalimbali yanayojengwa ndani ya nyumba (Gim) ili tuweze kuwa na afya bora tuweze kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, nayazungumza haya ikiwa machache ya yale ambayo tumeyajadili katika kipindi cha miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, leo hii nihitimishe hotuba yangu kwa kueleza hayo kwa kifupi kwa kuwatakia safari njema Waheshimiwa Wabunge wanaporejea majimboni kwao, kuwaeleza wananchi mambo mengi yaliyojiri hapa Bungeni hususan kuhusu manufaa ya Bajeti na Miswada tuliyoipitisha. Waelezeeni wananchi matarajio yetu kwao na kuwasihi waendeleo kutuunga mkono kwenye jitihada zetu za kuwawekea mazingira wezeshi ya kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusisitiza ushirikiano baina ya Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri

zetu katika ufuatiliaji wa fedha za maendeleo tunazopeleka kwenye Halmashauri ili zifanye kazi iliyokusudiwa. Aidha, naitakia maandalizi mema timu yetu ya Bunge itakayoshiriki kwenye mashindano ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakatayofanyika mwaka huu hapa mjini Dodoma. Tunayo imani kubwa na timu yetu kwani ni timu imara, timu bora yenye wachezaji mahiri na mwaka huu tutabakiza vikombe vyote hapa Tanzania. Tunawasahi mtuwakilishe vizuri kama kawaida yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa, napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 5 Septemba, 2017 siku ya Jumamne saa tatu asubuhi tutakapokutana tena katika ukumbi huu mkubwa wa kimataifa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli, sijawahi kuona hoja imeungwa mkono kwa kiwango hiki tena kwa pande zote mbili. Kwa uungwaji mkono huu sidhani kama ina haja hata ya kuhoji, lakini kwa vile Kanuni inanilazimisha nifanye hivyo, basi sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wabunge kwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba ambayo ameitoa hivi sasa ya kuliahirisha Bunge hadi tarehe aliyoitaja. (*Kicheko/Makofi*)

(Hoja ilitolewa iliamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Nitatoa shukrani baada ya muda si mrefu kwa niaba yenu, lakini nitumie muda huu mfupi kutoa waraka wa Spika Na.3 wa mwaka 2017 na waraka huu ni kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wangu wa kuunda Kamati Maalum itakayotathmini mfumo wa uchimbaji, usimamizi, umiliki na udhibiti wa madini ya almasi nchini kisha kuandaa mapendekezo mahususi kwa ajili ya kuishauri Serikali

kuhusiana na uendeshaji bora wa biashara ya madini ya almasi nchini.

Chimbuko la jambo hili ni tarehe 12 Juni, nilipohudhuria pale Ikulu kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge wakati ripoti ya pili ya Mwenyekiti wa Kamati Maalum Profesa Nehemia Osolo ambayo ilikuwa ikiangalia masuala ya kiuchumi na kisheria kuhusu usafirishaji wa makinikia, ikitolewa pale niliahidi kwamba na sisi tutaangalia kwenye eneo la madini ya almasi na kwa hatua hii mkumbuke kwamba tulishaunda Kamati ya kuangalia madini ya *Tanzanite* hapo kabla.

Pili, sababu ya kufanya hivi ni malalamiko ya wananchi ikiwa ni pamoja na Kamati ya Nishati na Madini ambayo pia imekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuhusiana na eneo hili. Kutokana na mazingira niliyokwishayaeleza hapa kabla, nimeunda Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi, Umiliki, Udhibiti, wa Madini ya Almasi Nchini kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016. Kamati hiyo naipa hadidu za rejea zifuatazo:-

- (i) Wachambue taarifa za Tume na Kamati mbalimbali zilizowahi kuundwa na Serikali kwa ajili ya kushughulikia mfumo wa uchimbaji, usimamizi, umiliki na udhibiti wa madini ya almasi nchini na kuona mapendekezo hayo kwa namna gani yanaweza kuhuishwa na Serikali kwa mazingira ya sasa.
- (ii) Kutathimini mfumo uliopo wa uchimbaji, usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini ya almasi nchini na kuanisha manufaa ambayo Serikali inapata na hasara ambazo tunapata kutegemeana na uwekezaji uliopo katika madini hayo hivi sasa.
- (iii) Wabainishe na kushauri kuhusu utaratibu bora *best practice* unaoweza kutumika katika

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kusimamia uwekezaji, uchimbaji na biashara ya madini ya almasi nchini.

- (iv) Kushughulikia jambo lolote linalohusiana na mfumo wa uchimbaji, usimamizi na udhibiti wa madini ya almasi nchini.

Waheshimiwa Wabunge Kamati hii Maalumu ninayoiunda leo itakuwa na wajumbe tisa niliowateua kwa kuzingatia vigezo vya taaluma, uzoefu, pande za Muungano, jinsia na uwakilishi wa Vyama hapa Bungeni. Kamati hiyo itafanya kazi kwa muda wa siku 30 kuanzia watakapoitwa na Katibu wa Bunge na kituo kikuu cha kazi yao kitakuwa ni hapa Bungeni Dodoma.

Itakapobidi Kamati hiyo itaweza kufanya ziara popote pale nchini watakapoona inafaa kwenda, lakini pia nitakuwa tayari kuwawezesha Kamati hii kusafiri nje ya nchi popote pale watakaponishauri kwamba ni muhimu wafanye hivyo ili kuweza kutekeleza vema majukumu yake.

Kamati hiyo itashauriwa kwa karibu na sekretarieti ambayo itaundwa na Katibu wa Bunge na maelezo ya ziada watapewa wakati watakapoitwa wakati wowote kuanza kazi yao. Wabunge hao tisa ambao nimewateua ni Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi wa CHADEMA; Mheshimiwa Shally Joseph Raymond wa CCM; Mheshimiwa Ali Abdalla Rashid wa CUF; Mheshimiwa Allan Joseph Kiula wa CCM, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo wa CCM; Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali wa CUF; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa wa CCM; Mheshimiwa Adamson Emmanuel Mwakasaka wa CCM; na ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa ni Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. Uamuzi huu nimeutoa leo tarehe 5 Julai, 2017. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua tuliyoifikia kwa niaba yenu wote nitoe shukrani nyingi sana, tulipofika hapa mwisho kwa ushirikiano mkubwa sana ambao kwanza nimeupata toka kwa wasaidizi wangu hapa mezani Mheshimiwa Naibu Spika Dkt. Tulia Ackson, ahsante sana.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mwenyekiti ahsante sana. Mheshimiwa Zungu, ahsante sana. Mheshimiwa Najma Giga, nakushukuru sana. Kwa kweli wamenisaidia mno mno peke yangu nisingeweza miezi hii yote mitatu kunyoosha mambo hapa, kwa hiyo, ahsanteni sana tuendelee kufanya kazi kwa pamoja.

Pia kwa niaba ya Wabunge wote tumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ametuwezesha sana kuhakikisha kwamba Bunge hili linaendelea kila wakati na Miswada mbalimbali ambayo tumeipitisha hapa ameisaini kwa haraka bila kusita na tunaendelea kufanya kazi na Serikali yake ambayo iko hapa kwa ushirikiano mkubwa, kwa hiyo, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Kipekee tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye pia ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana umetupa kila aina ya ushirikiano usiku na mchana, kwa kweli bila ushirikiano huo tusingeweza kufanikiwa kufika hapa mwisho kwa salama na amani. Niwashukuru sana Mawaziri wote wa Wizara mbalimbali, Manaibu Waziri na Maofisa wenu ambao katika kipindi hiki cha bajeti kila mmoja wenu alikuja hapa mbele, mkaeleza mambo ya Wizara zenu, mmechambua, mmetufafanulia, kuna wakati lugha zetu hazikuwa nzuri sana, lakini mmetuvumilia. Tunasema ahsanteni sana, mwendelee na moyo huo.

Niwashukuru wajumbe wote wa Kamati mbalimbali na Wenyeviti wenu ambao kupitia Kamati zenu, Kamati zote zilifanya kazi yaani moja au nyingine na wakati mwingine Kamati ya Bunge zima tukakutana hapa nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani ahsanteni sana kwa changamoto ambazo mmetupatia mara kwa mara, zimetusaidia sana katika kuendesha shughuli hapa, nasema ahsanteni sana na tuendelee na utaratibu huo, kwa sababu kwa pamoja tunaweza.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Naomba niwashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge ambao wamekuwa washauri wangu wa karibu. Tumekutana asubuhi, tumekutana mchana, tumekutana jioni, tumekutana usiku, tumekutana kwa vikao vya dharura, tumekuatana kila tulipohitaji kukutana na mahudhurio yalikuwa ni mazuri sana. Nawashukuruni sana Kamati ya uongozi na Kamati nyingine zote ambazo sijaweza kuzitaja hapa ambazo zimewezesha kazi zetu kuwa nzuri. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba niwashukuru sana Katibu wa Bunge na timu yake, hapa mezani, pamoja na watumishi wote wanao fanyakazi chini ya Ofisi ya Katibu wa Bunge, watumishi wa Bunge tunasema ahsanteni sana, sana. *(Makofi)*

Pia *support team* zote ambazo zilikuwepo hapa Bungeni muda wote, walinzi waliotulinda kuanzia milangoni na maeno mengine yote wamehakikisha tuko salama, mpaka tunapoondoka hakuna Mbunge aliyepoteza kiungo chake chochote cha mwili, kwa maana ya kupoteza jicho, sikio au mkono, ni kwa sababu ya usalama wa hali ya juu ambao tumekuwa tukipatiwa hapa sote kwa pamoja.

Vile vile niwashukuru Waandishi wa Habari na wadau wengine wote ambao wamefanya *covering* ya shughuli za Bunge katika kipindi chote ambacho tumekuwa hapa Bungeni. Nasema kwa wote hao ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mwisho niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Wabunge mtakapokuwa mkisafiri kurudi majumbani, mtufikishie salamu zetu kwa wapiga kura wenu na mwende mfafanue mambo yote haya ambayo tumeyajadili kwa muda wote huu na namna gani wananchi wanaweza kufaidika na maamuzi ambayo tumeyafanya ya aina mbalimbali hapa katika mjengo.

Kwa kumalizia niwahakikishie, nilimwomba kwa niaba yenu Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango asilale usiku wa leo na kwa kweli amekesha, basi katika kukesha kwake, natumaini

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge mmenielewa. Tumwombee tu na yeye anapokwenda likizo kule Buhigwe basi aende salama. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya hapo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tusimame tulipo ili tuweze kupata wimbo wa Taifa, wimbo wa Taifa tafadhali.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mkiwa mmesimama sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe iliyotajwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsanteni sana.

(Saa 6.45 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Septemba, 2017, Saa tatu Asubuhi)